NISHATI | HABARI ZA NISHATI


News Bulletin

www.nishati. go.tz | Wizara ya Nishati | wizara_ya_nishati_tanzania | @Nishati2017 | Wizara ya Nishati

Toleo Namba 11 Februari 1-29, **2020**

## MIAKA MINNE YA SERIKALI YA AWAMU YA TANO


# NISHATI YAJIVUNIA MAFANIKIO



- Ongezeko la megawati 480 za umeme katika gridi ya Taifa
- Bilioni 138 zimeokolewa kwa kuachana na matumizi ya mitambo mikubwa ya kufua umeme wa mafuta
- Uwepo wa ziada ya umeme usiopungua megawati 280 kwa siku
- Kusitisha uagizaji vifaa vya umeme nje ya nchi
- TANESCO - kutoka kampuni inayopata hasara na kuwa inayotengeneza faida na kujiendesha pasipo ruzuku
- Ongezeko la asilimia 400 uunganishaji umeme vijijini
- Gesi asilia imefikia futi za ujazo trilioni 57.54
- Uwepo wa mafuta yanayotosheleza mahitaji pamoja na akiba

UK. 2

## WAZIRI KALEMANI AWEKA JIWE LA MSINGI UJENZI WA NJIA YA KUSAFIRISHIA UMEME BULYANHULU - GEITA



JARIDA HILI LINATOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, 40474 Dodoma

# NISHATI YAJIVUNIA MAFANIKIO MIAKA MINNE YA SERIKALI YA AWAMU YA TANO

*Na Veronica Simba – Dar es Salaam*

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani amefanya mkutano na waandishi wa habari na kueleza mafanikio ya sekta ya nishati, yaliyopatikana katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Mkutano huo ulifanyika Ofisi ndogo za Wizara jijini Dar es Salaam, Februari 2, 2020 na kuhudhuriwa pia na Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu, Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Leonard Masanja, pamoja na viongozi mbalimbali wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

Akielezea mafanikio hayo, Waziri Kalemani aliyagawa katika sehemu nne ambazo ni hali ya upatikanaji umeme nchini, usambazaji umeme vijijini, matumizi ya rasilimali ya gesi asilia pamoja na hali ya upatikanaji mafuta nchini.

Yafuatayo, ndiyo aliyoyaeleza Waziri kwa kila sehemu:

**Hali ya upatikanaji umeme nchini**

- Hali ya upatikanaji umeme nchini imeendelea kuimarika siku hadi siku. Tunao umeme wa kutosha kwa sasa. Mwaka 2015 tulikuwa na megawati 1,038 za umeme katika gridi ya Taifa. Leo hii tuna jumla ya megawati 1,602.34. Tumeongeza zaidi ya megawati 480 mpya na tumekuwa na ziada ya umeme usiopungua megawati 280 kila siku.



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) kuhusu mafanikio ya sekta ya nishati katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Tano. Mkutano huo ulifanyika ofisi ndogo za Wizara jijini Dar es Salaam, Februari 2, 2020.*

- Tumeimarisha miundombinu ya uzalishaji umeme kwa kuongeza njia kuu za kusafirisha umeme ambazo hazikuwepo huko nyuma. Mwaka 2016 tulikamilisha mradi wa kusafirisha umeme mkubwa wa kilovoti 400, umbali wa kilomita 670 kutoka Iringa kupitia Dodoma – Singida hadi Shinyanga.

- Pia, tulikamilisha mradi wa kusafirisha umeme mkubwa wa kilovoti 220 kutoka Makambako kupitia Madaba hadi Songea, umbali wa kilomita 250.

- Tumeendelea kujenga njia za kusafirisha umeme (kilovoti 132) mahala ambapo hazikuwepo kabisa mathalani kutoka Mbagala – Mkuranga – Nanjilinji Mtwara kupitia Lindi, umbali wa kilomita 5.2.

- Tumeendelea kuunganisha maeneo mengi ambayo hayakuwa kwenye gridi ya Taifa, hasa yaliyokuwa yanatumia mashine za kufua umeme wa mafuta.

- Tumeondoa takribani vituo 12 vilivyokuwa vikitumia mafuta ambavyo baadhi yake ni Ngara, Biharamulo, Songea, Mbinga, Namtumbo, Ludewa na Nyakato. Tumeokoa pesa nyingi ambazo zilikuwa zinatumika kwa ajili ya kununua mafuta katika maeneo hayo.

- Pia, tumeondoa mitambo mikubwa ya IPTL (megawati 103), Aggreko (megawati 48) na Symbion (megawati 120-129) ambapo tumeokoa takribani shilingi bilioni 138. Tulipoondoa mitambo hiyo, tuliweza kuokoa kwa mwezi shilingi bilioni 6.9 zilizokuwa zinatumika kwa ajili ya uendeshaji wake.

- Vilevile, tumeendelea kuunganisha maeneo mbalimbali katika gridi ya Taifa na kuokoa shilingi bilioni 121. Maeneo hayo ni Tunduru, Mnazimmoja mkoani Lindi kuelekea Luangwa, umbali wa takribani kilomita 80 (kilovoti 132), Liwale, Masasi na Nanyumbu.

- Mwaka 2015, transfoma zilizokuwa zimefungwa nchini kote zilikuwa 12,000.2 lakini leo hii, jumla ya transfoma 23,000.56 zimefungwa nchini sawa na ongezeko la zaidi ya asilimia 100) Pia, tumeendelea na ukarabati wa transfoma zilizokuwa mbovu.

- Mwaka 205, tulikuwa na nguzo za umeme zilizojengwa nchini milioni 1.1. Leo, tuna zaidi ya nguzo milioni 3.7 zilizotumika hivyo tumeongeza usambazaji umeme katika maeneo mengi hivyo kuimarisha kabisa hali ya upatikanaji wau meme nchini.

- Mwaka 2017 tuliweka mkakati wa kiserikali kuhakikisha kwamba shughuli zote za usambazaji na ujenzi wa kupeleka umeme kwa wananchi, zinafanyika kwa haraka. Njia pekee ilikuwa ni kuhakikisha vifaa vinapatikana ndani ya nchi hivyo tulisitisha rasmi uagizaji vifaa hivyo kutoka nje ya nchi.

- Wakati huo tulikuwa na kiwanda kimoja cha kuzalisha transfoma, sasa viko vinne. Uwezo wetu wa ndani ilikuwa ni transfoma 97, leo hii ni 21,000 ingawa mahitaji yetu ni 14,000 kwa sasa. Kwahiyo transfoma zilizopo ni nyingi hadi zinabaki ziada.

- Pia, mwaka 2017 tulisitisha uagizaji wa nguzo kutoka nje ya nchi. Wakati huo, mahitaji yetu ya nguzo yalikuwa milioni 1.2 na uwezo wetu wa ndani ulikuwa 800,000 hivyo zilikuwa hazitoshi. Leo, tuna viwanda 10 ambavyo vinazalisha nguzo zaidi ya milioni

ENDELEA UK. 4

# MAONI/KATUNI





# BODI YA UHARIRI

**Mhariri**
**Veronica Simba**
(Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini)

**Waandishi**
**Veronica Simba**
**Teresia Mhagama**
**Zuena Msuya**
**Hafsa Omar**

**Msanifu Kurasa**
**Lucas Gordon**



Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018
Nukushi: +255-26-2320148 au

Fika Ofisi ya Mawasiliano Mtumba Dodoma, S.L.P. 2494, 40474 Dodoma

*www.nishati. go.tz*
*Wizara ya Nishati*
*@Nishati2017*
*wizara_ya_nishati_tanzania*
*Wizara ya Nishati*


## NJIA YA KUSAFIRISHIA UMEME BULYANHULU HADI GEITA ITAWAKOMBOA WANANCHI

Moja ya habari kubwa katika Jarida letu hili ni kuhusu tukio la uwekaji jiwe la msingi ujenzi wa mradi wa njia ya kusafirishia umeme wa msongo wa kilovoti 220 kutoka Bulyanhulu mkoani Shinyanga hadi Geita.

Imeelezwa kuwa tukio hilo muhimu lilifanyika Januari 4, 2010 ambapo Waziri mwenye dhamana na sekta ya nishati, Mheshimiwa Dkt Medard Kalemani ndiye hasa aliyehusika katika uwekaji jiwe hilo la msingi.

Tunaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Nishati kwa kuamua kuutekeleza Mradi huo ambao unahusisha pia ujenzi wa vituo vya kupoza umeme katika eneo la Bulyanhulu, wilayani Kahama na katika Mkoa wa Geita, pamoja na kusambaza umeme katika vijiji 10 vinavyopitiwa na mradi huo.

Kwa kutekeleza Mradi huo, wananchi wa wilaya za Kahama, Geita, Chato, Biharamulo na Ngara watanufaika kwani lengo lake ni kuimarisha upatikanaji wa nishati ya umeme katika maeneo hayo pamoja na kuunganisha Mkoa wa Geita katika Gridi ya Taifa.

Aidha, imebainishwa kuwa mbali na wananchi wa wilaya hizo kunufaika, migodi ya madini iliyopo katika mikoa husika ambayo ni Geita Gold Mine (GGM), Bulyanhulu na STAMIGOLD itanufaishwa na mradi huo pia.

Ndiyo maana sisi wa Nishati News Bulletin tumewiwa kutoa pongezi kwa serikali, kwa maana manufaa ya mradi huo hayaishii kwa wananchi kupata nishati ya umeme wa uhakika bali yanaenda mbali zaidi, ambapo kwa uwepo wa umeme huo, hakuna shaka miradi mingi ya kimaendeleo itaanzishwa na hivyo kuzinufaisha jamii husika na Taifa kwa ujumla.

Upatikanaji wa umeme wa uhakika ni shauku na hitaji la kila mwananchi mpenda maendeleo. Hivyo basi, wananchi nasi kwa upande wetu tunawajibika kuunga mkono jitihada za serikali yetu kwa kuhakikisha tunakuwa mabalozi na walinzi wa miundombinu inayowekezwa kwa gharama kubwa.


Tutambue kwamba, kuruhusu watu wasio wema kuhujumu miundombinu hiyo katika maeneo yetu ni sawa na kuruhusu umaskini kwetu sisi wenyewe.

Hakuna shaka kuwa, kwa mikakati hii inayotekelezwa na serikali, hususan katika miradi mbalimbali ya nishati; na kwa kasi ya utekelezaji wake; hakika ndani ya kipindi kifupi tutashuhudia maendeleo makubwa kwenye sekta husika.

Dalili njema tayari zinaonekana dhahiri kwani hata sasa tumeendelea kushuhudia mapinduzi makubwa ya kimaendeleo katika sekta ya nishati. Miradi mbalimbali mikubwa inatekelezwa nchi nzima mijini na vijijini; sote tu mashahidi.

Ndiyo maana tunasema, miradi yote ya umeme inayotekelezwa na serikali ukiwemo wa njia ya kusafirishia umeme wa msongo wa kilovoti 220 kutoka Bulyanhulu mkoani Shinyanga hadi Geita, itawakomboa wananchi.

# Katunika Ki-nishati





*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kulia) akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) kuhusu mafanikio ya sekta ya nishati katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Tano. Mkutano huo ulifanyika ofisi ndogo za Wizara jijini Dar es Salaam, Februari 2, 2020. Kushoto ni Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu.*

2.5 wakati mahitaji yetu ni chini ya milioni 2 kwa mwaka.

- Hii imesaidia sana kutengeneza ajira kwa watanzania. Zaidi ya watanzania 3,000 wameajiriwa kutokana na uwepo wa viwanda hivi vipya. Aidha, tumeokoa shilingi bilioni 162.23 kwa kutumia nguzo za ndani ya nchi.

- Kwa upande wa mita za LUKU, awali hatukuwa na viwanda hapa nchini. Mwaka 2017 tulisitisha kuagiza mita hizo kutoka nje ya nchi. Kwas asa tuna viwanda vikubwa vitatu vya kuzalisha mita za LUKU. Mahitaji yetu ni mita milioni 1.56 wakati uwezo wa kuzalisha ni zaidi ya mita milioni 2.5.

- Aidha, tulikuwa na kiwanda kimoja cha nyaya za umeme. Leo tunavyo zaidi ya vinne. Mahitaji yetu ni kilomita 149,000 kwa mwaka wakati uwezo wa kuzalisha ni kilomita 250,000.

- Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lilikuwa linapata hasara wakati ule kiasi cha shilingi milioni 439 lakini leo shirika halina hasara na linatengeneza faida. Kwa mwaka huu wa fedha, shirika limelipa gawio kwa serikali kiasi cha shilingi bilioni 1.43.

**Usambazaji umeme vijijini**

- Usambazaji umeme vijijini umeenda kwa kasi kubwa sana. Mwaka 2010, vijiji vilivyokuwa na umeme ni 562, mwaka 2015 vijiji 2,018 na leo hii tumefikia vijiji 8,517 kati ya 12, 268 vilivyopo nchini. Vijiji takribani 7,000 vimepelekewa umeme ndani ya miaka minne ambapo ni sawa na ongezeko la asilimia 400.

- Baada ya Juni mwaka huu, tunatarajia vitabaki vijiji 1,822 tu ambayo ni sawa na chini ya asilimia 15 ya vijiji vyote nchini. Ifikapo Juni 31, 2021 hakutakuwa na kijiji ambacho hakijafikiwa na umeme.

- Aidha, mwaka 2015 hatukuwa na Wilaya iliyokamilika kuunganishiwa umeme katika vijiji vyake vyote. Leo hii tunazo jumla ya Wilaya 34 nchini ambazo vijiji vyake vyote vimepata umeme.
Mwaka 2015, Taasisi za Umma zilizokuwa zimefikiwa na umeme zilikuwa 3,200 lakini leo idadi ya taasisi hizo imefikia 11,070 sawa na ongezeko la asilimia 500.
Kwa nchi za Afrika Mashariki, Tanzania inaongoza kwa kupeleka umeme vijijini kuliko nchi nyingine.

Matumizi ya gesi asilia

- Tunayo gesi ya kutosha nchini. Jumla ya gesi tuliyonayo ni futi za ujazo trilioni 57.54. Mwaka 2010 mahitaji yetu ya gesi yalikuwa futi za ujazo milioni 40. Mwaka 2019 mahitaji yetu yalikuwa futi za ujazo milioni 80 na sasa mahitaji yetu ni futi za ujazo milioni 200 kwa siku.

- Kati ya hizo, futi za ujazo milioni 135 zinatumika kuzalisha umeme na zilizobaki zinatumika katika viwanda na matumizi mengine ya ndani.

- Tumeunganisha viwanda vikubwa zaidi ya 48 katika mtandao wa gesi na zoezi linaendelea. Aidha, magari zaidi ya 250 kwa sasa yanatumia gesi nchini na wananchi zaidi ya 500 wanatumia gesi asili kupikia.

**Upatikanaji wa mafuta nchini**

- Hali ya upatikanaji wa mafuta nchini inaimarika siku hadi siku. Mwaka 2014 tulikuwa na utaratibu wa kuingiza mafuta kibinafsi. Serikali ikaanzisha Wakala wa Kuingiza Mafuta kwa Pamoja (PBPA).

- Mwaka 2015, uwezo wetu wa Bandari kupakua mafuta ulikuwa tani 165,000 na tulikuwa na bandari moja tu. Baada ya miaka miwili, tukaongeza bandari mbili zenye uwezo wa kupakua mafuta tani 45,000 kila moja.

- Hiyo imefanya kwa ujumla wake, bandaro zetu kuwa na uwezo wa kupakua mafuta tani 255,000.

- Tuna akiba ya mafuta kiasi cha kutosha ambapo kwa upande wa dizeli akiba tuliyonayo leo ni lita milioni 197.21 inayoweza kutosheleza mahitaji kwa zaidi ya siku 26. Petroli ziada ya lita milioni 97.2 inayotosheleza mahitaji ya zaidi ya siku 38, mafuta ya ndege ziada ya lita 30.18 yanayotosha kwa siku 58 na mafuta ya taa lita laki 6.6

- Vifaa vyetu vya kuhifadhi mafuta nchini kwa sasa vina uwezo wa kuhifadhi lita bilioni 1.3 kutoka uwezo wa zamani wa lita milioni 900.



*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (kushoto) na Kamishna wa Petroli na Gesi, Adam Zuberi wakifuatilia mkutano wa Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya sekta ya nishati katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Tano. Mkutano huo ulifanyika ofisi ndogo za Wizara jijini Dar es Salaam, Februari 2, 2020.*

# WAZIRI KALEMANI AWEKA JIWE LA MSINGI UJENZI WA NJIA YA KUSAFIRISHIA UMEME BULYANHULU - GEITA

*Hafsa Omar - Geita*

Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani, Januari 4, 2020 aliweka jiwe la msingi ujenzi wa mradi wa njia ya kusafirishia umeme wa msongo wa kilovolti 220 kutoka Bulyanhulu mkoani Shinyanga hadi Geita.

Katika tukio hilo, aliambatana na Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, Mkuu wa Mkoa wa Geita Mhandisi Robert Luhumbi na viongozi mbalimbali wa Serikali na vyama vya siasa.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri Kalemani alisema ujenzi wa mradi huo ulianza Januari 2019 na unatarajiwa kukamilika Mei mwaka huu (2020) ambapo zaidi ya vijiji 47 vitanufaika na mradi huo mkubwa utakaogharimu zaidi ya shilingi bilioni 50.

Alisema, mradi huo utapeleka umeme kwenye wilaya zote za mkoa huo na mikoa jirani na kuwezesha kutatua kero ya kukatika kwa umeme inayosababishwa na uwepo wa miundombinu isiyo imara.

Akieleza zaidi, alisema sehemu kubwa ya makusanyo ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), yanatokana na viwanda, hivyo dhamira ya Serikali ni kupeleka umeme kwenye viwanda vyote na migodi iliyopo nchini, huku akiwataka watanzania wajitokeze kuwekeza kwenye viwanda mkoani humo.



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akisalimiana na Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu alipowasili kwenye tukio la uwekaji wa jiwe la msingi ujenzi wa mradi wa njia ya kusafirishia umeme wa msongo wa kilovolti 220 kutoka Bulyanhulu Shinyanga hadi Geita.*

Akielezea mafanikio ya sekta ya nishati nchini, Dkt. Kalemani alisema TANESCO imefanikiwa kuunganisha na gridi ya Taifa maeneo mengi zaidi nchini ambayo yalikuwa yanatumia mitambo ya mafuta mazito. Aidha, aliongeza kwamba, vifaa vyote vya uunganishaji umeme kwa sasa vinapatikana nchini hali ambayo imesaidia wananchi kupata umeme kwa haraka.

Pia, aliongeza kuwa tayari takribani vijiji 8,818 vimeunganishwa na umeme na kuanzia Februari 2020, kazi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote nchini itaanza rasmi.

Vilevile, alielezea hatua ambazo zitachukuliwa na Serikali kuhakikisha nishati ya mafuta ya petroli na mafuta ya taa inafika vijijini ambapo alisema ameshatoa utaratibu kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kufanya mapitio ya kanuni na taratibu za uazishwaji wa vituo vya mafuta. "Lengo na dhamira ya Serikali ni kupeleka vituo vya mafuta vijijini mpaka kwenye vitongoji."

"Tumejiwekea miaka mitatu ijayo kila anayeanzisha kituo cha mafuta mjini, kama anaanzisha vituo vitatu, kimoja akipeleke kijijini ili kupunguza ukataji wa miti ovyo na kupunguza hatari ya kuungua kwa nyumba kwa baadhi ya watu wanaobeba mafuta kwenye madumu ya maji na kupeleka kwenye nyumba zao," alisema.



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akifanya mahojiano na mwandishi wa habari wa TBC.*



*Kutoka kulia Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, Mkuu wa Mkoa wa Geita Mhandisi Robert Luhumbi na Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu wakipiga makofi kwenye tukio la uwekaji wa jiwe la msingi ujenzi wa mradi wa njia ya kusafirishia umeme wa msongo wa kilovolti 220 kutoka Bulyanhulu Shinyanga hadi Geita.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, akipiga ngoma pamoja na kikundi kilichotoa burudani kwenye tukio la uwekaji wa jiwe la msingi ujenzi wa mradi wa njia ya kusafirishia umeme wa msongo wa kilovolti 220 kutoka Bulyanhulu Shinyanga hadi Geita.*

# MATUKIO PICHANI





*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza na wananchi kabla ya kuweka jiwe la msingi ujenzi wa mradi wa njia ya kusafirishia umeme wa msongo wa kilovolti 220 kutoka Bulyanhulu Shinyanga hadi Geita.*



*Mafundi wakiendelea na ujenzi wa mradi wa njia ya kusafirishia umeme wa msongo wa kilovolti 220 kutoka Bulyanhulu Shinyanga hadi Geita.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akikata utepe kuashiria uwekaji wa jiwe la msingi kwenye wa mradi wa njia ya kusafirishia umeme wa msongo wa kilovolti 220 kutoka Bulyanhulu Shinyanga hadi Geita.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kushoto), Mkuu wa Mkoa wa Geita Mhandisi Robert Luhumbi (kulia) wakiweka jiwe la msingi kwenye wa mradi wa njia ya kusafirishia umeme wa msongo wa kilovolti 220 kutoka Bulyanhulu Shinyanga hadi Geita.*



*Wananchi waliohudhuria kwenye sherehe za uwekaji jiwe la msingi kwenye wa mradi wa Njia ya kusafirishia umeme wa Msongo wa Kilovolti 220 kutoka Bulyanhulu Shinyanga hadi Mkoani Geita.*









*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani na Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu wakiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi na watumishi mbalimbali wa Wizara na Taasisi zake.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (katikati-waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Wawakilishi kutosha Shirika la Maendeleo la Japani (JICA), Wakuu wa Taasisi ya Nishati na Uchumi kutoka Japani, baadhi ya Viongozi Wakuu wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake, baada ya Naibu Waziri kufungua mkutano wa wadau hao uliofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni.*

# MIKOA MITANO SASA KUTUMIA GESI ASILIA

***Zuena Msuya – Dar es Salaam***

Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu, amesema tayari Serikali imekamilisha mpango wa awali wa kusambaza gesi kwenye mikoa mitano ili kuhakikisha kuwa Tanzania inatumia rasilimali hiyo inayochimbwa nchini katika kuimarisha uchumi wa viwanda.

Mgalu alisema hayo wakati akifungua mkutano wa wadau wa kujadili mpango wa kuhamasisha matumizi ya gesi asilia nchini, uliofanyika jijini Dar es Salaam, Januari 17, 2020.

Alisisitiza kuwa, mpango huo ni matokeo ya utafiti wa miaka mitatu, uliofanywa na Serikali kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan (JICA).

Aliitaja mikoa hiyo kuwa ni Arusha, Dodoma, Tanga, Kilimanjaro na Morogoro.

Aidha, alieleza kuwa lengo la serikali ni kuhakikisha mikoa yote Tanzania inapata nishati hiyo kwa matumizi mbalimbali.

"Tanzania tumegundua gesi asili yenye futi za ujazo trilioni 57; hii sasa tunaitengenezea mkakati wa matumizi yake."

Kwa mijiibu wa takwimu zilizopo, mpaka sasa gesi asilia inayochimbwa nchini inazalisha megawati 892.72 za umeme sawa na asilimia 57 ya megawati zote zinazozalishwa nchini.

Akieleza zaidi, Naibu Waziri alibainisha kuwa, gesi asilia inatumika pia kwenye magari, ambapo alisema kwa Dar es Salaam, magari takribani 200 yanatumia gesi na miundombinu ya kusambaza gesi hiyo inaendelea kuboreshwa ili kuwasogezea huduma watumiaji.

"Gesi asilia inatusaidia pia kutunza mazingira hasa kwenye kupikia ambapo mpaka sasa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), limesambaza miundombinu ya gesi ya kupikia majumbani katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Dar es Salaam na Pwani," alisisitiza Mgalu.

Kuhusu matumizi ya gesi viwandani, alisema viwanda zaidi ya 50 vimeunganishwa na nishati hiyo.

Kwa upande wake, Kamishna wa Petroli na Gesi wa Wizara ya Nishati, Adam Zuberi alisema Tanzania ipo kwenye wakati sahihi hivyo jitihada za makusudi zinafanyika kufikisha gesi asilia kwenye mikoa yote Tanzania.

"Tupo katika muda muafaka wa utafiti huu unaolenga kuhakikisha kwamba mikoa yote nchini inapata na kutumia gesi asilia kwa njia bora na sahihi," alisema Zuberi.

Mshauri wa Taasisi ya Nishati na Uchumi kutoka Japan, Kensuke Kanekinyo alisema awamu ya kwanza ya mradi huo imetumia Dola Milioni mbili za Marekani kwa kipindi cha miaka mitatu.

Alisema gharama za mradi wote ni Dola milioni 250 zitakazotumika kupeleka gesi mikoa yote ya Tanzania.



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akifungua mkutano wa wadau wa kujadili mpango wa kuhamasisha matumizi ya gesi asilia nchini, uliofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni.*



*Kamishna wa Petroli na Gesi, Adam Zuberi akizungumza na waandishi wa wabari wakati wa mkutano wa wadau wa kujadili mpango wa kuhamasisha matumizi ya gesi asilia nchini, uliofanyika jijini Dar es Salaam, hivi karibuni.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (kulia) akipokea jarida maalumu lenye taarifa mbalimbali zinazohusu Shirika la Maendeleo la Japani, (JICA) kutoka kwa mwakilishi wa Shirika hilo, Naofumi Yamamura, wakati wa mkutano wa wadau wa kujadili mpango wa kuhamasisha matumizi ya gesi asilia nchini, uliofanyika jijini Dar es Salaam, Januari 17, 2020*

# Mradi wa REA III mzunguko Pili kuanza Februari 2020



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akitoa taarifa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu hali ya upatikanaji wa fedha za miradi ya umeme vijijini katika kipindi cha nusu mwaka wa fedha 2019/2020. Kulia kwake ni Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu na kushoto kwake ni Kaimu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja.*



*Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakiwa katika kikao na Wizara ya Nishati na Taasisi zake kilicholenga kujadili hali ya upatikanaji wa fedha za miradi ya umeme vijijini katika kipindi cha nusu mwaka wa fedha 2019/2020.*

**Teresia Mhagama - Dodoma**

Imeelezwa kuwa, Mradi wa usambazaji umeme vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili, (Turnkey Phase III-Round II) utaanza kutekelezwa mwezi Februari, 2020 ambao utakamilisha lengo la Serikali la kupeleka umeme katika vijiji 12,268 ifikapo mwaka 2021.

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani alisema hayo wakati akitoa taarifa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu hali ya upatikanaji wa fedha za miradi ya umeme vijijini katika kipindi cha nusu mwaka wa fedha 2019/2020.

Katika kikao hicho aliambatana na Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, Kaimu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, Menejimenti ya Wizara pamoja na Wenyeviti wa Bodi na Menejimenti za Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Dkt. Kalemani alisema kuwa, mradi huo utasambaza umeme katika vijiji 1,822 ambavyo havikuwepo katika mradi wa usambazaji umeme vijijini wa Awamu ya Tatu mzunguko wa kwanza ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Juni mwaka huu.

Akitoa takwimu za usambazaji umeme vijijini, Dkt Kalemani alisema kuwa hadi kufikia mwezi Disemba 2015, jumla ya vijiji 2,018 vilikuwa na umeme na hadi kufikia Januari 10, 2020 jumla ya vijiji 8,408 vimepatiwa umeme ambayo ni sawa na asilimia 69.

Vilevile, alisema kuwa kutokana na miradi mbalimbali ya usambazaji umeme vijijini inayoendelea, inatarajiwa kuwa, kufikia mwezi Juni mwaka 2020, jumla ya vijiji 10,446 vitakuwa vimesambaziwa umeme.

Aidha, kuhusu wakandarasi wanaosuasua katika utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini, alisema kuwa, tayari wameshaandikiwa barua za kusudio la kusitisha mkataba na kampuni hizo zimepewa siku 60 za kurekebisha mapungufu la sivyo hatua zaidi za kimkataba zitachukuliwa.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Amos Maganga, aliieleza Kamati hiyo kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umeme vijijini ukiwemo wa kusambaza nishati jadidifu katika maeneo yaliyo mbali na gridi ya Taifa pamoja na visiwa.

Kuhusu mradi huo, alisema kuwa, Serikali kupitia Mfuko wa Nishati Vijijini kwa kushirikiana na Serikali za Sweden na Uingereza umetoa ruzuku kwa kampuni binafsi 14 ili kuvipatia umeme vijiji 119 kutokana na vyanzo vya nishati jadidifu ambapo vijiji 95 vimepelekewa umeme.

Kuhusu kupeleka umeme visiwani, Maganga alisema kuwa, jumla ya visiwa 22 kati ya 196 vimesambaziwa umeme kupitia mradi wa usambazaji umeme wa Awamu ya Tatu na kwamba visiwa vyote vitasambaziwa umeme ifikapo mwaka 2021.

Aidha, kuhusu suala la usambazaji umeme kwenye Taasisi za umma, alisema kuwa, hadi kufikia Disemba 2015 jumla ya Taasisi 4,036 ziliunganishiwa umeme na hadi kufikia Disemba 2019 jumla ya taasisi 11,070 zimesambaziwa umeme.

Katika kikao hicho, Kamati ya Bunge iliipongeza Wizara ya Nishati pamoja na Taasisi zake kwa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umeme ukiwemo wa Julius Nyerere (MW 2115). Aidha, Wajumbe wa Kamati hiyo walitoa maoni mbalimbali yatakayoboresha sekta ya nishati nchini.



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dunstan Kitandula akizungumza jambo katika kikao kati ya Kamati hiyo na Wizara ya Nishati na Taasisi zake kilicholenga kujadili hali ya upatikanaji wa fedha za miradi ya umeme vijijini katika kipindi cha nusu mwaka wa fedha 2019/2020. Kushoto kwake ni Katibu wa Kamati hiyo, Felister Mgonja.*



*Watendaji wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake wakiwa katika kikao na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini (hawapo pichani), kilichohusu hali ya upatikanaji wa fedha za miradi ya umeme vijijini katika kipindi cha nusu mwaka wa fedha 2019/2020.*

# MRADI WA 'PERI-URBAN' KUONGEZA IDADI YA WATUMIAJI UMEME NCHINI - MGALU

***Hafsa Omar - Pwani***

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu amesema mradi wa umeme wa 'Peri-Urban' umebuniwa kwa mara ya kwanza nchini ili kukidhi haja ya ongezeko la mahitaji ya nishati hiyo kwa maeneo ambayo yanakua kwa kasi.

Aliyasema hayo, Januari 23, mwaka huu wakati akiwa kwenye ziara ya ukaguzi wa kazi ya usambazaji umeme wilayani Kisarawe, Mkoa wa Pwani.

Akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kuhitimisha ziara yake ya ukaguzi wa mradi wa 'Peri-Urban' mkoani humo, alisema, tangu mradi huo ulivyozinduliwa, wananchi wameupokea vizuri na wameonesha mwamko mkubwa wa kuunganisha huduma hiyo.

"Imepita miezi minne tangu mradi huo uanzishwe; tukaona kuna kila sababu ya kuja kukagua hali ya utekelezaji inavyoendelea, ukizingatia kuwa ni mradi mkubwa kwa sababu unatarajia kuunganisha wananchi wengi."

Alisema, serikali ina matumaini kuwa ndani ya miezi mitano iliyobaki kazi itaendelea vizuri na kwa kasi kubwa, kwakuwa vifaa vingi vinavyotekeleza mradi huo vinazalishwa nchini ambapo alimtaka mkandarasi anayehusika kufanya kazi usiku na mchana ili kumaliza mradi kwa wakati.

Mgalu aliwataka wasambazaji wa nguzo, nyaya na transfoma nchini kutumia vizuri fursa waliyopewa na Serikali kwa kusambaza vifaa hivyo kwa wakati pamoja na kutoa ushirikiano kwa wakandarasi ili miradi yote iweze kukamilika ndani ya muda uliopangwa.

Aidha, alisema mradi huo pia utaiwezesha Serikali kufikia lengo lake la kuviunganishia umeme vijijini vyote ifikapo Juni, na kuongeza kwamba, Wizara ina matumaini makubwa kuwa lengo hilo litafikiwa kupitia miradi mbalimbali inayoendelea kutekelezwa ikiwemo ya REA III, 'Peri-Urban' na Ujazilizi.

Aidha, Naibu Waziri aliwatoa hofu wananchi wote ambao wamelipia huduma ya umeme wa REA III, mzunguko wa kwanza ambao katika orodha ya wateja wa awali, walizidi idadi iliyopo kwenye mkataba wa mradi huo hivyo kushindwa kuunganishiwa umeme; kuwa wataunganishiwa huduma hiyo mara tu baada ya mkataba wa nyongeza utakapoanza kazi.

"Hapa Kisarawe wapo wananchi takribani 239 walishalipa lakini walishindwa kuunganishwa kwa wakati kwasababu idadi iliyohitajika kwa Kisarawe ilishakamilika. Hivyo, niwatoe hofu wote waliolipa na ambao hawajalipa kwamba uunganishaji umeme utaanza ambapo kwa sasa REA wapo kwenye manunuzi ya vifaa."

Sambamba na hayo, pia alieleza kuwa Serikali mwaka huu itaingia mkataba na wazalishaji binafsi, kuzalisha umeme wa megawati 950 kutoka kwenye vyanzo vya upepo, jua na makaa ya mawe lakini pia kazi inaendelea ya utafiti wa chanzo cha umeme wa joto ardhi.



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kuhitimisha ziara yake ya ukaguzi wa kazi ya usambazaji umeme wilayani Kisarawe, Mkoa wa Pwani.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akisaini kitabu cha wageni alipowasili kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe kwa lengo la kupata taarifa ya maendeleo ya sekta ya nishati. Kulia ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Jokate Mwegelo.*




*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akitoa taarifa ya miradi ya umeme inayotekelezwa wilayani Kisarawe, alipotembelea Ofisini kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, akiwa katika ziara ya kazi hivi karibuni.*

# Kamati ya Bunge yapongeza Wizara kuiboresha TANESCO



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akitoa taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa majukumu na upatikanaji wa fedha katika Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Kampuni ya Uendelezaji wa Rasilimali ya Jotoardhi Tanzania (TGDC) katika kipindi cha nusu mwaka wa 2019/2020 kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini katika kikao kilichofanyika jijini Dodoma.*

***Teresia Mhagama - Dodoma***

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kupitia Mwenyekiti wake, Dunstan Kitandula imewapongeza viongozi wa Wizara ya Nishati, kwa usimamizi wao unaoendelea kuboresha utendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na kuhakikisha kuwa Shirika hilo linatekeleza majukumu yake ipasavyo na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Pongezi hizo zimetolewa Januari 18, 2020 jijini Dodoma wakati wa kikao cha Kamati hiyo na watendaji wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake wakiongozwa na Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani na Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu.

Kikao hicho kilikuwa mahsusi kwa ajili ya utoaji wa taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa majukumu na upatikanaji wa fedha kwa TANESCO na Kampuni ya Uendelezaji wa Rasilimali ya Jotoardhi Tanzania (TGDC) katika kipindi cha nusu mwaka wa 2019/2020.

"Tunaona jitihada zinazofanyika za kuiboresha TANESCO na sisi tunakupongeza Waziri na timu yako, lakini bado kuna vitu vya kurekebisha ikiwemo kuwafanya baadhi ya watumishi wa TANESCO kutoka kwenye ufanyaji kazi wa kimazoea unaotokana na kuona kuwa Shirika hili ni la umma na wawe na mtazamo wa kibiashara ambao utaliletea faida Shirika huku likitoa huduma bora kwa wananchi," alisema Kitandula.

Kitandula pia alisisitiza kuwa, kasi ya kuunganisha wananchi na huduma ya umeme iongezeke pamoja na uboreshaji wa utoaji wa taarifa kwa wananchi akitoa mfano kuwa, inapotokea changamoto ya umeme, wananchi wapewe taarifa ndani ya muda muafaka na kuwe na mawasiliano chanya kati ya mteja na watoa huduma wa TANESCO.

Aidha, Kamati ya Bunge iliipongeza TANESCO kwa kuacha kutegemea ruzuku kutoka serikalini ili kujiendesha na kwa mara ya kwanza imetoa gawio serikalini la shilingi bilioni 1.436 katika mwaka 2019.

Kuhusu TGDC, Kamati iliipongeza kampuni hiyo kwa jitihada zake za kuhakikisha kuwa Jotoardhi inaendelezwa na kusema kuwa kampuni hiyo ni muhimu katika uendelezaji wa rasilimali hiyo ambayo ni moja ya vyanzo vya nishati jadidifu nchini na itawezesha juhudi za Serikali za kuwa na umeme wa uhakika kwani Tanzania ina uwezo wa kuzalisha umeme wa Jotoardhi usiopungua megawati 5000.

Waziri wa Nishati, awali, alipata fursa ya kueleza hali ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme ambapo katika uzalishaji umeme alisema kuwa uwezo wa mitambo ya kufua umeme nchini umefikia jumla ya megawati 1,602.318 huku mahitaji ya juu katika mfumo wa gridi ya Taifa yakifikia megawati 1,120.12 ambayo yalifikiwa tarehe 27 Novemba, 2019.



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akitoa taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa majukumu na upatikanaji wa fedha katika Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Kampuni ya Uendelezaji wa Rasilimali ya Jotoardhi Tanzania (TGDC) katika kipindi cha nusu mwaka wa 2019/2020 kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini katika kikao kilichofanyika jijini Dodoma.*



*Watendaji wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati, wakiwa katika kikao na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. Kikao hicho kililenga kutoa taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa majukumu na upatikanaji wa fedha katika Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Kampuni ya Uendelezaji wa Rasilimali ya Jotoardhi Tanzania (TGDC) katika kipindi cha nusu mwaka wa 2019/2020 kilichofanyika jijini Dodoma.*



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dunstan Kitandula akizungumza jambo katika kikao kati ya Kamati hiyo na Wizara ya Nishati na Taasisi zake kilicholenga kupata taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa majukumu na upatikanaji wa fedha katika Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Kampuni ya Uendelezaji wa Rasilimali ya Jotoardhi Tanzania (TGDC) katika kipindi cha nusu mwaka wa 2019/2020. Kushoto kwake ni Katibu wa Kamati hiyo, Felister Mgonja.*



*Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji wa Rasilimali ya Jotoardhi Tanzania (TGDC), Mhandisi Kato Kabaka akitoa taarifa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu na upatikanaji wa fedha katika kampuni hiyo katika kipindi cha nusu mwaka wa 2019/2020.*

# SERIKALI YAOKOA TRILIONI 30 KWA KUTUMIA GESI ASILIA

***Hafsa Omar - Dodoma***

Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani amesema tangu mwaka 2004 ambapo gesi asilia ilianza kutumika kama nishati mbadala nchini, hadi kufikia Desemba 2019, Serikali imeokoa zaidi ya Dola za Marekani 13.048 ambazo ni sawa na shilingi trilioni 30.225.

Aliyasema hayo Januari 17 mwaka huu, alipokuwa akiwasilisha taarifa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kuhusu utekelezaji wa majukumu na hali ya upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).

Vilevile, alisema kuwa, ugunduzi wa gesi asilia nchini umeimarisha uzalishaji wa umeme nchini ambapo kwa sasa asilimia 57.02 ya umeme unaozalishwa nchini unatokana na nishati hiyo.

Aidha, Waziri alielezea maendeleo ya miradi mbalimbali ya utafutaji mafuta na gesi katika vitalu mbalimbali vya Mnazi Bay Kaskazini, Eyasi-Wembere na Namba 4/1B.

Kuhusu kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini, alisema kuwa, mradi huo unalenga kufanya utafiti wa mafuta na gesi asilia katika kitalu hicho kilichopo katika bahari ya kina kirefu kusini mwa Tanzania.



*Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, wakiwa katika kikao na watendaji wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake, kilicholenga kujadili kuhusu utekelezaji wa hali ya upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa kipindi cha nusu mwaka, kwa mwaka wa fedha 2019/2020.*



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (kushoto) akisikiliza maoni mbalimbali kutoka kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini (hawapo pichani) mara baada ya kuwasilisha taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa hali ya upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa kipindi cha nusu mwaka, kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Kushoto kwa Waziri ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dkt. Adelardus Kilangi.*

"Kazi zilizotekelezwa hadi sasa ni pamoja na kukamilisha takwimu za mitetemo pamoja na uchambuzi wa kiufundi wa zabuni ya kumpata mshauri mwelekezi wa uchorongaji wa visima vya utafiti."

Aliongeza kuwa, kazi za uchorongaji katika Kitalu hicho unatarajiwa kuanza ifikapo Agosti, 2020 na kukamilika Oktoba, 2020.

Akielezea kuhusu mradi wa Eyasi-Wembere, Dkt Kalemani alisema kuwa, unalenga kufanya utafutaji wa mafuta ambapo kazi zilizotekelezwa hadi sasa ni pamoja na kukamilisha uchorongaji wa visima viwili vifupi vya utafutaji katika maeneo ya King'inila- Igunga na Nyaranja-Meatu kwa ajili ya kuchukua sampuli za miamba na kutoa elimu kwa jamii kuhusu mradi huo.

Alisema kuwa, kazi ya kuchoronga kisima cha tatu katika eneo la Luono-Iramba inaendelea na inatarajiwa kukamilika Februari 2020.

Kuhusu mradi wa utafutaji mafuta na gesi katika Kitalu Namba 4/1B kilicho katika bahari ya kina kirefu kusini mwa Tanzania, Dkt Kalemani alisema kuwa kazi ya ukusanyaji wa takwimu katika kitalu hicho itaanza mwezi Machi na kukamilika mwezi Juni 2020.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio alisema kuwa, kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Desemba 2019, Shirika hilo limekusanya zaidi ya shilingi bilioni 293 kutoka vyanzo vya ndani ikiwa ni sawa na asilimia 75 ya lengo la makusanyo ya nusu mwaka.

Aliongeza kuwa, mapato ya ndani yameongezeka kwa asilimia 6.4 yakilinganishwa na mapato ya shilingi bilioni 275.77 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2018/19.

Alisema, Shirika hilo linategemea vyanzo vya mapato ya ndani ambavyo ni pamoja na mauzo ya gesi asilia, mapato yatokanayo na shughuli za mkondo wa juu, gawio la uwekezaji Songas pamoja na vyanzo vingine.

# Migodi 136 nchini yaunganishiwa umeme

**_Zuena Msuya - Shinyanga_**

Imeelezwa kuwa Serikali imedhamiria kuwainua wachimbaji wadogo kwa kuwaunganishia huduma ya umeme katika migodi na mitambo ya kuchenjulia dhahabu ili kuwapunguzia gharama za uendeshaji na kupata faida kubwa zaidi.

Dhamira hiyo ilidhihirishwa na Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, Januari 24, 2020, wakati akiwasha umeme katika mgodi na mtambo wa kuchenjua dhahabu ambao ni wa 136 kuwashiwa umeme nchi nzima, uliopo katika Kijiji cha Mwabomba wilayani Kahama mkoani Shinyanga.

Dkt. Kalemani alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Tano kupitia sera ya uchumi wa viwanda imedhamiria kuwainua na kuwathamini zaidi wachimbaji wadogo kwa kuhakikisha inawaunganishia umeme wa bei nafuu wale wote wenye migodi na mitambo ya kuchenjua dhahabu, ili umeme huo uwarahisishie shughuli za uendeshaji na kuinua vipato vyao.

Alisema umeme katika sehemu za migodi utampunguzia mchimbaji mdogo gharama za uendeshaji na kupata faida ambayo pia atalipa kodi na tozo mbalimbali za serikali bila vikwazo na kuiongezea serikali mapato.

"Tutahakikisha migodi na mitambo yote ya kuchenjua dhahabu au madini ya aina yeyote ile hapa nchini inaunganishiwa umeme. Hii itasaidia pia kuwa na uchimbaji wa kisasa zaidi kwa kutumia teknolojia bora ambazo hazitaruhusu hata chembe ya madini yao kupotea; na teknolojia hizo ni rafiki kwa binadamu na mazingira kwa jumla. Bila umeme, teknolojia nyingine hawataweza kuzitumia," alisema Dkt. Kalemani.

Akizungumzia usambazaji wa umeme vijijini, Waziri aliliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuunganisha kata zote 20 katika Wilaya ya Kahama, ambazo hazijaunganishwa kabla ya mwezi Aprili mwaka huu.

Alieleza kuwa wananchi hawataki kusikia habari ya aina yoyote juu ya umeme, zaidi ya kuona unawaka ndani ya majumba yao na hakuna sababu ya msingi ya kuwafanya wananchi hao wakose umeme kwa kuwa tayari fedha zipo na vifaa vyote vinapatikana hapa nchini na watalaamu wa kazi hiyo wapo.

Mapema akiwa katika ziara hiyo wilayani Nyang'hwale, mkoani Geita, Dkt. Kalemani, aliwaagiza watendaji wa TANESCO, kukamilisha ufungaji wa mashineumba (Transfoma) na kuwasha umeme katika mgodi wa Nyamigongo ambao hutumia zaidi ya shilingi milioni 120 kwa mwezi ikiwa ni gharama za kununua mafuta ya kuendesha shughuli za uzalishaji ambapo ukitumika umeme gharama yake itakuwa takribani shilingi milioni 80 tu.

Akifafanua zaidi, Waziri alisema mashineumba watakayofunga siyo kwamba itamnufaisha mwekezaji huyo pekee, bali zaidi ya vijiji 20 vinavyomzunguka vitatumia mashineumba hiyo. Alisema, kwa mantiki hiyo, shirika hilo litapata faida kubwa itakayowawezesha kuendelea kusambaza umeme na kuboresha miundombinu iliyochakaa ama kuharibika.

Kwa upande wao, wamiliki wa migodi hiyo, wameishukuru serikali kwa kuwathamini wachimbaji wadogo ambao kwa mujibu wao, walikuwa kama wametelekezwa katika kutatuliwa matatizo na changamoto mbalimbali zinazowakabili ikiwamo kuboreshwa kwa shughuli zao za uchimbaji ili uwe wa manufaa zaidi.

Vilevile, akiwa wilayani Nyang'hwale, Waziri aliwasha umeme katika Shule ya Msingi iliyoanzishwa mwaka 1958, takribani miaka 62 iliyopita.

Aidha, alitembelea eneo linalojengwa Makao Makuu ya Wilaya ya Nyang'hwale, Hospitali na majengo mengine ya serikali na kuagiza TANESCO kufunga mashineumba yenye uwezo mkubwa katika eneo hilo ili iharakishe shughuli za kiutendaji.

Pia, alimuagiza mkandarasi anayetekeleza mradi wa usambazaji umeme vijijini katika wilaya hiyo, kuongeza kasi ya kuunganishia umeme wateja waliolipia na kuongeza kasi ya usambazaji umeme katika vijiji wanavyotekeleza mradi huo pamoja na kuwasha umeme katika vijiji vitatu kila wiki.

Waziri alimtaka Mkandarasi kuondoa nguzo zilizorundikwa sehemu moja kwa muda mrefu na kuzisambaza katika maeneo mbalimbali zinapohitajika na endapo ni mbovu basi azirudishe alikozinunua ili wapatiwe nguzo zingine kulingana na makubaliano yanavyoelekeza.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya hiyo, Hamim Gwiyama alimhakikishia Waziri Kalemani kuwa kabla ya majengo hayo kukamilika watalipia gharama za uunganishaji umeme ili umeme huo pia usaidie shughuli za umaliziaji ujenzi wa majengo hayo.

Vilevile, aliahidi kuwa, wataendelea kulipia taasisi za umma kama shule, vituo vya afya na taasisi za dini zilizopo katika maeneo yao ili ziunganishiwe umeme.



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, akioneshwa jinsi umeme unavyosaidia kurahisisha kazi ya kuchenjua dhahabu kwa kutumia teknolojia ya kisasa katika mgodi wa Mwabomba wilayani Kahama mkoani Shinyanga.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, (kulia) akipitishwa na mmiliki mgodi na mtambo wa uchenjuaji dhahabu wa Mwabomba (kushoto) katika sehemu ya mtambo huo unaotumia umeme kuendesha shughuli za uchenjuji dhahabu kwa kutumia teknolojia ya kisasa ambayo ni rafiki kwa binadamu na mazingira.*

# MATUKIO PICHANI



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, (katikati) akikata utepe na kuwasha umeme katika mgodi na mtambo wa kuchenjua madini ya dhahabu wa Mwabomba wilayani Kahama mkoani Shinyanga.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, (aliyesimama) akizungumza katika kikao cha ndani na wafanyakazi wa TANESCO, REA, wakandarasi pamoja na viongozi wa wilaya ya Nyang'hwale alipofika kufanya kazi ya kukagua maendeleo ya usambazaji umeme wilayani hapo. Kulia ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Hamim Gwiyama na Mbunge wa Nyang'hwale, Husein Nassoro Amir.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, (katikati) akitembelea eneo litakalojengwa Makao Makuu ya Wilaya ya Nyang'hwale, Hospitali na majengo mengine ya serikali. Kulia ni Mbunge wa Jimbo la Nyang'hwale, Husein Nassoro Amir na Mkuu wa Wilaya hiyo Hamim Gwiyama.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, (kushoto) na Mkuu wa Wilaya ya Nyang'hwale, Hamim Gwiyama, wakikagua baadhi ya vyumba katika jengo litakalokuwa Makao Makuu ya Wilaya hiyo.*



*Mafundi wa TANESCO wakiendelea na kazi ya kufunga mashineumba (Transfoma) katika moja ya migodi ya dhahabu katika Wilaya ya Nyang'hwale.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, (katikati) akitoa maelekezo kwa watendaji wa TANESCO kuharakisha ufungaji wa mashineumba na kuwashwa umeme katika mgodi wa dhahabu wa Nyamigoro.*



*Wanafunzi wa Shule ya Msingi Bukwimba, wilayani Nyang'hwale mkoani Geita, wakifurahia kuwashwa kwa umeme katika shule yao iliyoanzishwa mwaka 1958 ikiwa ni takribani miaka 62 bila kuwa na umeme.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, (katikati), Mkuu wa Wilaya ya Nyang'hwale Hamim Gwiyama, na Mbunge wa Nyang'hwale, Husein Nassoro Amir wakiondoka katika Mgodi wa dhahabu wa Mwabomba, wilayani Kahama, baada ya kujiridhisha na kazi ya kufunga mashineumba (Transfoma) katika mgodi huo.*



Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga (katikati), akitoa maagizo kwa Mkandarasi anayetekeleza Mradi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Bulyanhulu hadi Geita, alipotembelea Mradi huo hivi karibuni.



Kazi ya uchimbaji wa msingi kwa ajili ya kusimika nguzo za chuma katika Mradi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Bulyanhulu hadi Geita ikiendelea. Taswira hii ilichukuliwa Januari 20, mwaka huu wakati Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga alipotembelea Mradi huo.

# USIMIKAJI NGUZO MRADI WA UMEME BULYANHULU -GEITA KUANZA FEBRUARI

***Na Mwandishi Wetu***

Kamishna Msaidizi wa Umeme Mhandisi Innocent Luoga, amefanya ziara ya kukagua utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 220 inayoanzia Bulyanhulu hadi Geita na kumtaka Mkandarasi kuanza kazi ya kusimika nguzo za chuma ifikapo Februari, 2020.

Mhandisi Luoga alifanya ziara hiyo Januari 20, 2020 kukagua Mradi huo ambao unahusisha pia ujenzi wa vituo vya kupoza umeme katika eneo la Bulyanhulu, wilayani Kahama na katika Mkoa wa Geita, pamoja na kusambaza umeme katika vijiji 10 vinavyopitiwa na mradi huo.

"Nimeridhishwa na kasi ya ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Bulyanhulu na Geita lakini sijaridhishwa na kazi ya usimikaji wa nguzo za kusafirisha umeme ambapo misingi 52 kati ya misingi 161 imekamilika na hakuna nguzo iliyosimamishwa.

Nawataka Mkandarasi na Mhandisi Mshauri kujipanga upya ili mradi huo wenye lengo la kuimarisha upatikanaji wa umeme katika wilaya za Kahama, Geita, Chato, Biharamulo na Ngara pamoja na kuunganisha Mkoa wa Geita katika Gridi ya Taifa ukamilike kwa wakati," alisema.

Aidha, Mhandisi Luoga alimuagiza Mkandarasi kufanya kazi siku zote, kuongeza idadi ya mafundi na vifaa maalum vya kuchimba katika miamba ili kuhakikisha nguzo zinaanza kusimamishwa ifikapo Februari 2020 na Mradi huo unakuwa tayari kusafirisha umeme.

Akitoa maelezo kwa Kamishna, Mhandisi wa Mradi Ramadhani Kidunda alisema Mradi huo unatarajiwa kukamilika tarehe 30 Mei 2020 na utahusisha pia kusambaza umeme katika vijiji 10 vinavyopitiwa na Mradi husika pamoja na vituo vya kupoza umeme katika eneo la Bulyanhulu na Geita.

Kamishna Luoga aliwataka Mameneja wa TANESCO wa Mikoa ya Shinyanga na Geita kuhakikisha wanafanya usanifu wa kutosha ili migodi iliyopo katika Mikoa hiyo ikiwemo Geita Gold Mining (GGM), Bulyanhulu na STAMIGOLD inapatiwa umeme wa uhakika pamoja na vijiji vyote vinavyopitiwa na Mradi huo ambavyo havina umeme na kuvipatia nishati hiyo kupitia Mradi huo bila kuruka kijiji chochote.

Aidha, aliitaka TANESCO kumsimamia Mkandarasi kikamilifu ili kuhakikisha Mradi unatekelezwa katika ubora na viwango vinavyotakiwa.

Katika ziara hiyo, Kamishna Msaidizi wa Umeme Mhandisi Innocent Luoga, aliambatana na Mhandisi wa Mradi huo, Ramadhani Kidunda, Meneja wa TANESCO wa Mkoa wa Shinyanga, Meneja wa Wilaya ya Kahama pamoja na Mkandarasi anayetekeleza Mradi huo ambaye ni M/s CAMC Engineering Co Ltd ya China na Mhandisi Mshauri M/s SHAKER kutoka Misri.







Hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Bulyanhulu. Taswira hizi zilichukuliwa Januari 20, mwaka huu wakati Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga alipotembelea Mradi huo.

# Wakandarasi Mradi wa Umeme Julius Nyerere watakiwa kuishi eneo la Mradi



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (wa pili-kulia) akikagua ubora wa kitasa cha mlango wa moja ya nyumba za kuishi wafanyakazi zilizokamilika kujengwa katika mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP).*



*Muonekano wa baadhi ya nyumba za wafanyakazi wanaotekeleza mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) zilizokamilika kujengwa katika eneo la mradi.*

***Zuena Msuya - Morogoro***

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani amewataka wakandarasi na wahandisi wanaotekeleza ujenzi wa mradi wa bwawa la kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya bonde la Mto Rufiji wa Julius Nyerere (JNHPP) kuhamia na kuishi katika eneo la mradi kuanzia Januari 13, 2020, baada ya ujenzi wa nyumba za wafanyakazi kukamilika.

Aidha, amewataka wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) pamoja na wahandisi washauri wa mradi (TECU) kuhamia katika eneo la mradi kuanzia mwezi Februari mwaka huu baada ya nyumba zao kukamilika pia.

Dkt. Kalemani alitoa agizo hilo, Januari 12, 2020, alipofanya ziara ya kumi ya kukagua maendeleo na hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa mradi huo, tangu kusainiwa kwa mkataba na mkandarasi kuanza kufanya kazi za mradi huo uliopo Rufiji.

Alisema kuwa, kuanzia sasa hakuna sababu ya wafanyakazi wanaotekeleza mradi wa JNHPP, kuishi mbali na eneo la mradi kwa kuwa tayari ujenzi wa nyumba za wafanyakazi umekamilika.

"Hatupendi kuona wafanyakazi wa mkandarasi wanaishi Dar es Salaam, wakati kazi inafanyika Rufiji. Kuanzia kesho (Januari 13, 2020), wakandarasi wote wahamie eneo la mradi, na wale wafanyakazi wa TANESCO na TECU wao watahamia kuanzia mwezi ujao baada ya nyumba zao kukamilika," alisema Dkt. Kalemani.

Alisema tayari nyumba nane zenye uwezo wa kubeba wafanyakazi 192 zimekamilika huku akibainisha kuwa lengo la nyumba zinazojengwa ni kubeba zaidi ya wafanyakazi 400 watakaokuwa wakiishi katika eneo la mradi.

Katika ziara hiyo pia, Waziri alimtaka mkandarasi wa mradi huo kuanza kupeleka mitambo tisa ya kufua umeme (Turbine) pamoja na vipuri vingine vinavyohitajika katika eneo la mradi kwa kuzingatia makubaliano ya mkataba. Pia, aliwataka TANESCO pamoja na TECU kuwa wazalendo katika kuhakiki ubora wa mitambo hiyo kwa manufaa ya Taifa na kuhakikisha inafika eneo la mradi kwa wakati uliopangwa.

Vilevile aliendelea kupiga marufuku wafanyakazi wageni kufanya kazi zinazoweza kufanywa na watanzania zikiwemo za vibarua, ulinzi, wauza vyakula na kadhalika na kwamba yeyote atakayekaidi maagizo hayo atachukuliwa hatua kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba.

"Tunataka kuona walinzi ni SUMA JKT au Jeshi la Wanyamapori. sitegemei kuona mlinzi kutoka nje ya Tanzania akiwa pale getini na endapo atakuwepo basi achukuliwe hatua. Nawaagiza Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, simamieni hili," alisisitiza Dkt. Kalemani.

Akizungumzia usafishaji wa eneo la mradi, Dkt. Kalemani alitoa miezi miwili kwa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), TANESCO, TECU na wote wanaohusika katika kusafisha eneo la mradi lenye ukubwa wa kilometa 914 kuharakisha utekelezaji wa mradi huo kwa kuwa mpaka sasa kazi hiyo haijafanyika.

Aidha, aliwaagiza TFS kuwatumia watu wenye sifa na uwezo mkubwa wa kufanya kazi hiyo kwa kasi na kiwango cha hali ya juu. Hata hivyo, aliwashauri kufanya mazungumzo na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ili kutekeleza kazi hiyo kwa haraka.

Katika ziara hiyo, Dkt. Kalemani, alitembelea eneo la ujenzi wa bwawa, madaraja, mitambo ya kusaga kokoto na kuchanganya zege na sehemu ya kujenga mitambo tisa (turbines) ya kufua umeme.

Dkt. Kalemani alisema kuwa ameridhishwa na maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo ambao katika kila hatua ya Mpangokazi, utekelezaji wake umekamilika kwa asilimia 95 kwa kila kazi iliyopangwa, ambapo kwa ujumla katika hatua za awali za utekelezaji wa mradi huo umekamilika kwa asilimia 5 na kazi zinaendelea vizuri. Mradi huo unatarajiwa kukamilika Juni 14, 2022.

Katika utekelezaji wa ujenzi wa mradi huo, tayari Mkandarasi alishalipwa kiasi cha shilingi Trilioni 1.5 ikiwa ni malipo ya awali.


Mapema akiwa njiani kuelekea eneo la mradi, Dkt. Kalemani alizungumza na wakazi wa kijiji cha Kisaki na kuwaahidi kutatua malalamiko yao kuhusu utaratibu wa kuwapatia vijana ajira ambao wengi wao walikuwa wakiulalamikia.

Hata hivyo, aliwataka vijana wanaopata kazi katika mradi huo, kufanya kazi kwa kujituma na kuzingatia mikataba ya kazi, badala ya kutoroka na kuacha kufanya kazi walizopewa.

# MATUKIO PICHANI



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza mara baada ya kutembelea daraja la muda lililojengwa katika bonde la mto Rufiji kurahisisha usafirishaji wa vifaa na mahitaji mbalimbali ng'ambo ya mto ili kutekeleza shughuli za ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme.



Mwonekano wa mtambo wa kusaga mawe ili kupata kokoto za ukubwa wa aina tofauti kulingana na mahitaji, zitakazotumika katika shughuli za ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (wa pili-kushoto) akikagua sehemu ya eneo litakapojengwa bwawa la kuzalisha umeme katika bonde la mto Rufiji.



Vibarua wakiendelea na shughuli mbalimbali za ujenzi kulingana na Mpangokazi wa utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa bwawa la kuzalisha umeme.





Daraja la muda lililojengwa kurahisisha usafirishaji wa vifaa na mahitaji mbalimbali katika upande wa pili wa mto katika eneo litakapojengwa bwawa la kuzalisha umeme.



Kazi ya kupasua miamba na kuondoa vifusi ikiendelea kulingana na Mpangokazi wa utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa bwawa la kuzalisha umeme.




Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (aliyeshika kipaza sauti), akizungumza na wakazi wa kijiji cha Kisaki baada ya kusikiliza malalamiko yao mbalimbali ikiwepo fursa za upatikanaji ajira katika mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP).

# USAMBAZAJI UMEME HAUTASIMAMA - MGALU

***Hafsa Omar - Pwani***

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, amesema kazi ya kusambaza umeme nchini ni endelevu na Serikali inatarajia kuanza rasmi kusambaza umeme kwenye vitongoji vyote nchini mara tu baada ya kumaliza kusambaza umeme kwenye vijiji vyote ifikapo Juni 2021.

Aliyasema hayo, Januari 21, 2020, kwa nyakati tofauti akiwa kwenye ziara ya ukaguzi wa kazi ya usambazaji umeme katika vijiji vya Kimange, Kibindu, Lupungwi na Talawanda, wilayani Bagamoyo, Mkoa wa Pwani.

Alisema jukumu la Serikali ni kutoa huduma kwa wananchi wake na Serikali ya Awamu ya Tano imeazimia kutoa huduma ya nishati ya umeme kwa Watanzania wote.

"Kazi ya kupeleka umeme vijijini tunaikamilisha mapema Juni 2021, kazi inayofuata ni kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote nchini kwahiyo ni kazi ya kata mti panda mti," alisema.

Pia, aliwataka wananchi kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kuunganisha umeme kwenye nyumba zao, kwasababu Serikali inatumia fedha nyingi kuhakikisha miundombinu ya umeme inafika sehemu zote bila kuangalia umbali wa maeneo.

Aliongeza kuwa, maeneo mengi ya Chalinze, mara ya baada kusambaziwa umeme wawekezaji wengi wamejitokeza kuwekeza kwenye maeneo hayo ambapo hapo awali walishindwa kufika katika maeneo hayo kwasababu ya changamoto ya upatikanaji wa umeme lakini kwa sasa fursa nyingi za kiuchumi zimejitokeza wilayani humo.

Naibu Waziri Mgalu, aliendelea kuwahimiza viongozi mbalimbali wa Halmashauri, Wenyeviti na Madiwani kuendelea kutenga fedha za kuunganisha umeme kwenye Taasisi za umma na kwamba suala hilo ndiyo liwe kipaumbele chao mara tu baada ya miundombinu ya umeme kufika kwenye maeneo yao.

Aidha, alilipongeza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa kazi nzuri wanayoifanya ya usambazaji umeme, na kumtaka Meneja wa Mkoa huo kuhakikisha hakuna kijiji kitakachorukwa kwenye mradi wa REA III, ili wananchi wote wafaidike na huduma hiyo.



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mkoa wa Pwani, Martin Madulu alipokuwa katika ziara ya kazi wilayani humo kukagua kazi ya usambazaji umeme.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (wa kwanza-kushoto) akiwa kwenye kituo cha afya cha Kimange wilayani Bagamoyo pamoja na viongozi mbalimbali wa kijiji hicho wakati alipokwenda kukagua kazi ya usambazaji umeme kwenye taasisi za umma.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akizungumza na wananchi wa kijiji cha Kimange wilayani Bagamoyo mara baada ya kukagua kazi ya usambazaji umeme kijijini humo.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akisalimiana na wananchi wa Kijiji cha Lupungwi wilayani Bagamoyo alipowasili kijijini hapo kwa ajili ya ukaguzi wa kazi ya usambazaji umeme.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akisaini kitabu cha wageni alipowasili katika kijiji cha Kimange wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani. Naibu Waziri alifanya mkutano wa hadhara kijijini hapo.*



*Wananchi wa kijiji cha Talawanda wilayani Bagamoyo wakimsikiliza Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (hayupo pichani) kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika kijijini humo wakati Naibu Waziri alipofika kijijini hapo kukagua kazi ya usambazaji umeme.*



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, akikata utepe kabla ya kuwasha rasmi umeme katika Mgodi wa dhahabu wa Aljazeera uliopo katika kijiji cha Mgusu, wilayani Geita Vijijini hivi karibuni akiwa katika ziara ya kazi.

*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, akioneshwa namna ambavyo dhahabu imechenjuliwa kwa kutumia teknolojia rafiki na mazingira inayotumia umeme, katika Mgodi wa Dhahabu wa Aljazeera, wilayani Mugusu, Geita Vijijini. Waziri aliwasha rasmi umeme katika Mgodi huo hivi karibuni, akiwa katika ziara ya kazi.*



# Dkt. Kalemani aagiza Mkandarasi akamatwe kwa kutapeli wanakijiji

*Zuena Msuya - Geita*

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani ameviagiza vyombo vya ulinzi na usalama kwa kushirikiana na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kumsaka na kumkamata Mkandarasi anayefanya kazi ya kusuka mfumo wa nyaya za umeme kwenye majengo, Kampuni ya Cyber kwa kosa la kutapeli wananchi, kutomaliza kazi kwa wakati na kuondoka eneo la kazi pasipo kutoa taarifa.

Kampuni hiyo ya Cyber ilikuwa ikifanya kazi husika katika baadhi ya nyumba za wakazi wa Kijiji cha Ibisabageni, Wilaya ya Geita Vijijini, mkoani Geita kwa makubaliano na wananchi hao.

Dkt. Kalemani alitoa agizo hilo baada ya kusikiliza malalamiko yaliyotolewa na baadhi ya wananchi hao, wakati wa ziara yake ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji umeme vijijini, katika wilaya hiyo, Januari 23 mwaka huu.

Akizungumza kwa niaba ya wanakijiji wenzake, Samuel Mayala alimweleza Waziri kuwa, mkandarasi huyo alikuwa akiwatoza fedha za kazi hiyo kulingana na ukubwa wa nyumba ya mteja.

Mayala aliendelea kusema kuwa, mkandarasi huyo baada ya kupokea fedha kutoka kwa wananchi, alikuwa akifanya kazi hiyo bila kuikamilisha na wengine walilipia gharama hizo pasipo kufanyika kazi yoyote na baadaye alitoweka katika eneo la kijiji bila taarifa zozote.

"Mheshimiwa Waziri, kwa mfano mimi aliniambia nilipie shilingi laki mbili na themanini, nikalipa, ikabaki hamsini, akasema hawezi kumaliza kazi mpaka nimalize kulipia, nikamaliza kulipia lakini mpaka sasa sijamuona na hakumaliza kazi yangu," alisema Mayala.

Kufuatia malalamiko hayo, Dkt. Kalemani aliwataka watendaji wa TANESCO kuhakiki na kuwathibitisha wakandarasi wote wanaofanya kazi ya kutandaza nyaya katika nyumba za wanchi ili kuwaepusha na matapeli pamoja na vishoka.

Sambamba na hilo, aliwataka wananchi wote kuwatumia wakandarasi wanaotambuliwa na wenye uthibitisho kamili kutoka TANESCO.

Katika ziara hiyo, Dkt. Kalemani aliwasha umeme katika vijiji vya Ibisabageni na Bujuru vilivyopo Geita Vijijini pamoja na mgodi wa dhahabu wa Aljazeera uliopo katika kijiji cha Mgusu, Wilaya ya Geita Mjini.

Meneja wa Mgodi huo, Charles Nsangi aliishukuru Serikali ya Awamu ya Tano, kupitia Wizara ya Nishati kwa kuwaunganishia umeme ambao utapunguza gharama za uendeshaji tofauti na ilivyokuwa hapo awali wakati wakiendesha shughuli za mgodi huo kwa kutumia mafuta mazito.

Alisema kuwa kabla ya kufungiwa umeme, walikuwa wakitumia lita 40 za mafuta kwa siku kuendesha shughuli za mgodini, gharama ambayo ni kubwa kulingana na faida ya uzalishaji; lakini baada ya kupata umeme gharama zimepungua na kupata faida zaidi.



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kulia) akitoa maelekezo kwa viongozi wenye dhamana ya kufikisha umeme kwa wananchi, kutoka kulia kwa Waziri ni Mhandisi Edson Ngabo (Wizara ya Nishati), Mhandisi Ernest Makale (Wakala wa Nishati Vijijini – REA) na Mhandisi Innocent Luoga (Wizara ya Nishati). Waziri alikuwa katika ziara ya kazi mkoani Geita hivi karibuni.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani,akielezwa namna mtambo unaotumia umeme kuendesha shughuli za uzalishaji katika mgodi wa Aljazeera katika kijiji cha Mgusu wilayani Geita Mjini.*

# MATUKIO *PICHANI*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akikata utepe kabla ya kuwasha umeme katika Shule ya Msingi Ibisabageni, wilayani Geita Vijijini hivi karibuni, akiwa katika ziara ya kazi.*



*Mwananchi kutoka kijiji cha Ibisabageni, wilayani Geita Vijijini (kushoto), akiwasilisha kwa niaba ya wenzake, malalamiko ya kutapeliwa fedha na mkandarasi Kampuni ya Cyber, mbele ya Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kulia). Waziri alikuwa katika ziara ya kazi kijijini hapo hivi karibuni.*



*Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Ibisabageni, Geita Vijijini, wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani alipofika katika shule yao kuwasha rasmi umeme, hivi karibuni akiwa katika ziara ya kazi.*




*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akiangalia vijana wanaofanya kazi ya kusambaza miundombinu ya umeme vijijini wakati wa ziara yake wilayani Geita Vijijini hivi karibuni.*



*Wakazi wa Kijiji cha Bujuru, Bukwimba wilayani Geita Vijijini, wakishangilia umeme kufikishwa kijijini kwao wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani hivi karibuni.*



*Diwani wa Kata ya Bujuru, Amina Sued (kushoto), akiteta jambo na Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, kabla ya kuanza mkutano na wanakijiji pamoja na kuwasha umeme katika kijiji hicho hivi karibuni.*



*Mmoja wa Wazee wa Kijiji cha Bujura, John Masanja, akipiga magoti kuonesha furaha yake na shukrani kwa Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, kufika kijijini hapo akiwa katika ziara ya kazi hivi karibuni. Ilielezwa kuwa Waziri Kalemani ni kiongozi wa kwanza wa kitaifa kutembelea kijiji hicho tangu kupatikana kwa Tanzania ipate uhuru.*

# NAIBU WAZIRI NISHATI AMTAKA MKANDARASI KUMALIZA KAZI KWA WAKATI



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akizungumza na wananchi wa Ngobanya, Kata ya Kimbiji, Wilaya ya Kigamboni, mkoani Dar es Salaam wakati wa ziara ya kukagua kazi ya kusambaza umeme mkoani humo Januari 22, 2020.*



*Wananchi wa Mtaa wa Kitonga, Kata ya Msongala, Wilaya ya Ilala mkoani Dar es Saalam, wakimsikiliza Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (hayupo pichani) katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika mtaa huo Januari 22, mwaka huu.*

***Hafsa Omar - Dar es Salaam***

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu amesema Serikali haitamuongezea muda Mkandarasi wa kampuni ya Namis anaye tekeleza Mradi wa umeme wa 'Peri-Urban' katika jimbo la Ukonga jijini Dar es Saalam.

Aliyasema hayo, Januari 22 mwaka huu, wakati alipokuwa akijibu hoja mbalimbali za wananchi wa Mtaa wa Kitonga, Kata ya Msongala, Wilaya ya Ilala, mkoani Dar es Salaam, akiwa kwenye ziara ya ukaguzi wa kazi ya usambazaji umeme mkoani humo.

Alisema kuwa, mkandarasi husika alipewa kutekeleza mradi huo baada ya kushinda vigezo vilivyohitajika na kwamba anatarajiwa kuukamilisha ndani ya muda uliopangwa ambao ni Mei mwaka huu.

"Niwatoe hofu na mtuamini kuwa tutakuja kuwasha umeme hapa Mei, katika maeneo yote, tena kwa mpigo. Tunataka vitendo. Mkandarasi tunakuomba ufanye kazi usiku na mchana, hatutaki tena kuja kusikiliza kero za mradi huu; imetosha."

Aidha,alisema Mkoa wa Dar es Saalam una uhitaji mkubwa wa umeme na kwamba Serikali imejipanga kikamilifu kusambaza nishati hiyo kwenye jiji hilo na maeneo mengine yote nchini.

Akieleza zaidi, alibainisha kuwa, sheria iliyounda Wakala wa Nishati vijijini (REA) imeipa majukumu ya kusambaza umeme vijijini tu, lakini Serikali kwa kuona umuhimu wa kusambaza umeme kwenye maeneo ambayo yapo kwenye manispaa, ambayo sio miji au vijiji ikaamua kuleta mradi huo wa 'Peri-Urban' ili wananchi wa maeneo hayo nao wapate huduma ya umeme kwa bei ya shilingi 27,000 tu.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri alilitaka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuendelea kuwaunganishia umeme wateja wengi ili Shirika liweze kutoa huduma kwa ufanisi na kujipatia mapato kupitia wateja hao.

Alieleza kuwa, Tanzania ndiyo nchi ya kwanza Afrika Mashariki kwa usambazaji umeme, na imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kupeleka umeme vijijini ambapo vijiji vingi nchini tayari vimeshapatiwa umeme.

Aliongeza kuwa, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kila kaya inapata nishati, ambazo ni kichocheo cha maendeleo. Alisema Wizara imejipanga kusambaza umeme na gesi, na tayari kazi ya usambazaji gesi majumbani imeanza katika maeneo ambayo bomba la gesi lilipopita na maeneo mengine mbalimbali nchini.

Katika ziara yake, Naibu Waziri pia alikagua maendeleo ya mradi wa 'Peri-Urban' katika mtaa wa Ngombani, Kata ya Kimbiji, wilayani Kigamboni.



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akisaini kitabu cha wageni kabla ya kuzungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara, Mtaa wa Kitonga, Kata ya Msongala, wilayani Ilala Mkoa wa Dar es Saalam, hivi karibuni.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akizungumza na watalaam mbalimbali wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mara baada ya kufanya ukaguzi wa kazi ya usambazaji umeme katika Mtaa wa Ngobanya, Kata ya Kimbiji, Wilaya ya Kigamboni, jijini Dar es Salaam.*

# Waziri wa Nishati awasha umeme Ibushi mkoani Tabora

*Zuena Msuya - Tabora*

Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani amewasha umeme katika Kijiji cha Ibushi pamoja na kukagua kazi ya usambazaji wa umeme vijijini katika Kijiji cha Majengo.

Dkt Kalemani alifanya kazi hiyo katika vijiji husika vilivyopo Wilaya ya Uyui mkoani Tabora, Januari 25, 2020.

Katika ziara hiyo Dkt. Kalemani aliwataka wananchi hao kutandaza mfumo wa nyaya za umeme katika nyumba zao na kulipia gharama ya uunganishwaji umeme kwa kuwa umeme huo utaunganishwa kwa wananchi wote kwa gharama nafuu ya shilingi 27,000 tu.

Aliwasisitiza kutumia wakandarasi walioidhinishwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), katika kazi ya kutandaza mfumo wa nyaya za umeme katika nyumba zao ili kukwepa kurubuniwa na vishoka.

Aidha, aliwataka kutolipia gharama za nguzo, LUKU wala nyaya katika zoezi zima la kuwekewa umeme zaidi ya bei elekezi iliyotolewa na serikali ya shilingi 27,000 tu.



*Vijana wa kijiji cha Majengo wilayani Uyui, mkoani Tabora wakiendelea na kazi ya kusimika nguzo za umeme katika kijiji hicho. Taswira hii ilichukuliwa wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), kijijini hapo hivi karibuni.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kulia) na Mbunge wa Jimbo la Tabora Kaskazini, Almas Maige (kushoto) wakimsikiliza Mwenyekiti wa Serikali ya Mitaa (hayupo pichani), akieleza kuhusu hali ya upatikanaji umeme katika kijiji cha Ibushi wilayani Uyui, mkoani Tabora, hivi karibuni.*



*Mbunge wa Tabora Kaskazini, Almas Maige akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Ibushi wilayani Uyui, mkoani Tabora wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani ya kukagua maendeleo ya usambazaji umeme katika kijiji hicho.*



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza na wanakijiji wa Ibushi (hawapo pichani), akiwa katika ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme vijijini, Wilaya ya Uyui, mkoani Tabora hivi karibuni.*



*Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Ibushi wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji umeme katika Wilaya ya Uyui, mkoani Tabora.*



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, akiwakabidhi kifaa cha Umeme Tayari (UMETA) wanafunzi wa shule ya Sekondari ya Ibushi pamoja na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, ili kitumike katika shule hiyo kwa ajili ya wanafunzi kujisomea nyakati za usiku. Waziri alikuwa katika ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme wilayani Uyui, mkoani Tabora.



Mmoja wa akina mama wa Kijiji cha Ibushi akiwa nje ya nyumba yake kabla ya Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, kuwasha umeme katika nyumba hiyo. Waziri alikuwa katika ziara ya kazi kukagua maendeleo ya usambazaji umeme wilayani Uyui, mkoani Tabora.



Mbunge wa Tabora Kaskazini, Almas Maige akishangilia baada ya Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, kukata utepe na kuwasha umeme katika kijiji cha Ibushi wilayani Uyui, mkoani Tabora akiwa katika ziara ya kazi hivi karibuni.



Wakazi wa kijiji cha Ibushi, wilayani Uyui mkoani Tabora, wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, wakati wa ziara yake wilayani humo hivi karibuni.



Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga (kushoto), akifuatilia maelekezo ya Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, aliyokuwa akiyatoa baada ya kufanya ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme katika kijiji cha Ibushi wilayani Uyui Mkoani Tabora hivi karibuni.

# MATUKIO *PICHANI*

## MATUKIO MBALIMBALI YA MKUTANO WA WADAU KUJADILI MPANGO WA KUHAMASISHA MATUMIZI YA GESI ASILIA NCHINI, ULIOFANYIKA JIJINI DAR ES SALAAM, JANUARI 2020. MKUTANO HUO ULIFUNGULIWA NA NAIBU WAZIRI WA NISHATI, SUBIRA MGALU.











# WAZIRI KALEMANI ATOA MAAGIZO MAZITO KWA WAKANDARASI WA UMEME VIJIJINI

- *Wenye utendaji duni wawajibishwe*
- *Wakamilishe kazi Aprili, 2020*
- *Wananchi visiwani watozwe bei ya umeme iliyopitishwa na serikali*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akizungumza na wakandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini, awamu ya tatu, mzunguko wa kwanza (REA III-Round 1), jijini Dodoma, Januari 29, 2020.*

**NA Veronica Simba – Dodoma**

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani amekutana na wakandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa kwanza na kuwapa maagizo mazito yanayolenga kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati na viwango stahiki.

Mkutano huo uliofanyika, Januari 29, 2020 jijini Dodoma, ulihudhuriwa pia na Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara husika, Mhandisi Leonard Masanja, Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti za Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) pamoja na wasimamizi wa miradi husika kutoka wizarani, TANESCO na REA.

Moja ya maagizo aliyoyatoa Waziri ni kwa watendaji wakuu wa TANESCO na REA, kuziwajibisha kampuni tatu za wakandarasi ambazo utendaji kazi wake hadi sasa uko chini ya wastani kwa mujibu wa mikataba yao waliyosaini.

Alizitaja kampuni hizo kuwa ni Urban & Rural Engineering Ltd ambayo utendaji wake katika wilaya za Kakonko na Kibondo mkoani Kigoma uko chini; JV Pomy Engineering Co. Ltd, Intercity Builders Ltd & Octopus Engineering Ltd (Kaliua, Tabora) pamoja na NIPO Group Ltd (Arusha).

Akifafanua, Waziri Kalemani alieleza kuwa, kampuni hizo tatu ni miongoni mwa kampuni saba ambazo zilibainika kufanya kazi chini ya kiwango na serikali ikatoa maelekezo kuwa zifanye marekebisho ya kuboresha utendaji wao ndani ya siku 14; hata hivyo ni kampuni nne tu kati ya hizo zilitimiza maelekezo husika.

"Nazidi kuelekeza; siku 14 mlizowapatia kwa barua zenu, kulingana na mkataba zikikamilika pasipo wao kurekebisha dosari hizo; chukueni hatua ya kufuta mikataba yao au kusitisha malipo yao pamoja na kutoa adhabu kulingana na mkataba ulivyo."

Sambamba na maagizo ya kuziwajibisha kampuni hizo zenye utendaji duni, Waziri alizipongeza kampuni tano ambazo zimefanya vizuri kwa kuvuka kiwango cha mkataba hadi kufikia sasa.

Alisema, kwa mujibu wa mkataba, wakandarasi wote wanapaswa kukamilisha kazi ifikapo Juni mwaka huu lakini kampuni hizo zimevuka lengo kwa baadhi yake kukamilisha kazi kwa asilimia 100 hadi sasa, ikiwa ni miezi mitano kabla ya makubaliano na nyingine kufikia kiwango cha juu kabisa zikielekea kukamilisha kazi husika ndani ya muda mfupi ujao.

Kampuni hizo ni STEG International Services waliotekeleza mradi kwa asilimia 100 katika mikoa ya Songwe na Mbeya; Sengerema Engineering Group Ltd, mkoani Pwani (zaidi ya 99%); Derm Electrics Ltd, wilayani Handeni (99.2%); JV White City International Contractors and Guangdong Co. Ltd, wilayani Simiyu (96%) pamoja na State Grid Electrical & Technical Work Ltd, mkoani Lindi (97%).

Maagizo mengine aliyotoa Waziri ni kwa kila mkandarasi kuhakikisha anakamilisha kazi katika eneo lake ifikapo Aprili mwaka huu ili miezi miwili inayosalia (Mei na Juni) itumike kukamilisha marekebisho madogo madogo kabla ya kukabidhi rasmi ifikapo Juni, 2020.

Sanjari na hilo, aliwataka mameneja wa TANESCO wa wilaya na mikoa pamoja na wahandisi wanaosimamia miradi husika, kuhakikisha ifikapo Februari 15, mwaka huu pasiwepo na nguzo iliyosimikwa ikiwa haijafungwa nyaya za umeme, pasiwepo na eneo la mradi lisilo na transfoma na pasiwepo na eneo la mradi ambalo wateja hawajaunganishiwa umeme.

Aidha, Waziri aliagiza kila mkandarasi kukabidhi Mpango-Kazi wake kwa uongozi wa TANESCO na REA pamoja na Wakuu wa Wilaya ambao unaainisha majina ya vijiji vitakavyounganishiwa umeme kila wiki, kuanzia sasa hadi mwezi Aprili, ambao ndiyo wa mwisho kwa kila mmoja kuwa amekamilisha kazi.

"Taarifa hizo ziwafikie Wakuu wa Wilaya kabla ya Februari 5, mwaka huu. Niwaombe Wakuu wa Wilaya mfuatilie utekelezaji

ENDELEA UK. 25



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akizungumza na wakandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini, awamu ya tatu, mzunguko wa kwanza (hawapo pichani), jijini Dodoma, Januari 29, 2010. Kushoto ni Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja na kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Wakili Julius Kalolo.*

# WAZIRI KALEMANI ATOA MAAGIZO MAZITO KWA WAKANDARASI WA UMEME VIJIJINI

wa kazi husika kama ambavyo taarifa itakuwa imeainisha. Mkandarasi akishindwa kutekeleza kama alivyoainisha, chukueni hatua za kumkamata," alisisitiza.

Katika hatua nyingine, Waziri alikemea tabia ya baadhi ya wakandarasi kutotekeleza kazi ipasavyo huku wakitoa kisingizio cha kutokuwa na vifaa. Alisema, wakandarasi wanapaswa kufahamu kuwa ununuzi wa vifaa ni jukumu lao maana wote wamelipwa na serikali ili kuwawezesha kutekeleza kazi zao ikiwemo hiyo ya ununuzi wa vifaa.

Vilevile, alitoa onyo kwa wapimaji wa miradi ya umeme (surveyors), hususan wale wanaokaa na fomu za wateja zaidi ya 10 kwa muda mrefu pasipo kwenda kutekeleza kazi husika, kuacha tabia hiyo mara moja vinginevyo watawajibishwa.

Waziri alitoa kalipio kwa mameneja wa TANESCO ambao kwa namna moja au nyingine wanaruhusu wananchi, hususan walioko maeneo ya visiwani kutozwa gharama kubwa za umeme na wazalishaji binafsi.

"Nimeambiwa baadhi ya visiwa ikiwemo Ukerewe, wananchi wanatozwa shilingi 2,500 kwa uniti moja ya umeme jambo ambalo siyo sawa maana bei iliyopitishwa na serikali kwa wananchi wote ambao matumizi yao hayazidi uniti 75 kwa mwezi ni shilingi 100 tu kwa kila uniti."

Hata hivyo, Waziri alizipongeza Bodi, Menejimenti na wafanyakazi wa TANESCO na REA kwa kufanya kazi nzuri hususan katika uunganishaji umeme katika maeneo mbalimbali nchini jambo ambalo liliungwa mkono na Naibu Waziri Mgalu wakati akifunga mkutano huo kwa niaba ya Waziri.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, Waziri na Naibu wake walisema pamoja na uwepo wa changamoto kadhaa katika utekelezaji wa miradi ya umeme lakini kwa kiasi kikubwa watendaji husika wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana.

"Kimsingi tunawahitaji sana. Tunahitaji sana ushirikiano wenu na kujitoa kwenu ili kwa pamoja tufanikishe azma ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt John Pombe Magufuli ya nchi kuwa ya uchumi wa viwanda. Hili linawezekana kwa uwepo wa umeme wa uhakika na wenye gharama nafuu," alisema Naibu Waziri.

Aidha, Naibu Waziri aliipongeza Bodi ya Wakurugenzi ya REA akisema inapaswa kuigwa kutokana na utendaji kazi wake mahiri. "Bodi hii inatembelea maeneo mbalimbali ya mradi na kukutana na watendaji wa pande zote zinazohusika ambazo ni serikali, wakandarasi, wauzaji na wazalishaji wa vifaa ili kujua changamoto zao na kuzitafutia ufumbuzi.

Naye Kaimu Katibu Mkuu, Mhandisi Masanja aliwaasa wakandarasi husika kuhakikisha wanaongeza nguvu katika kukamilisha idadi ya wananchi wanaopaswa kuunganishiwa umeme kwa mujibu wa mikataba yao badala ya kuunganisha wananchi wachache na kuhamia kijiji kingine.

Kwa upande wao, watendaji wakuu kutoka TANESCO, REA na wakandarasi husika waliahidi kutekeleza maagizo yote waliyopewa na Waziri.



*Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, akizungumza wakati wa mkutano wa Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kulia) na wakandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini (hawapo pichani). Katikati ni Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu. Mkutano huo ulifanyika jijini Dodoma, Januari 29, 2020.*



*Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Amos Maganga, akizungumza wakati wa mkutano wa Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani) na wakandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini (hawapo pichani). Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania, Dkt Tito Mwinuka. Mkutano huo ulifanyika Dodoma, Januari 29, 2020.*



*Badhi ya maafisa kutoka Wizara ya Nishati, Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na wakandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini wakifuatilia kikao cha Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani) na wakandarasi hao. Mkutano huo ulifanyika Dodoma, Januari 29, 2020.*









*Badhi ya maafisa kutoka Wizara ya Nishati, Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na wakandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini wakifuatilia kikao cha Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani) na wakandarasi hao. Mkutano huo ulifanyika Dodoma, Januari 29, 2020.*

# DKT KALEMANI AZINDUA MATUMIZI YA GESI ASILIA UDSM



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (wa nne kutoka kulia) akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa matumizi ya gesi asilia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Februari 1, 2020.*

**Veronica Simba – Dar es Salaam**

Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani amezindua matumizi ya gesi asilia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), katika hafla iliyofanyika Februari 1, 2020 ambapo kwa hatua hiyo ya awali, migahawa minne chuoni hapo imeanza kutumia huduma hiyo.

Akizungumza katika hafla hiyo ya uzinduzi, Dkt Kalemani alisema dhamira ya serikali ya kutumia gesi asilia inayopatikana nchini kwa maendeleo ya Taifa iko palepale tofauti na wanavyoamini baadhi ya watu kuwa nishati hiyo haipewi kipaumbele katika matumizi yake.

"Gesi hii tutaendelea kuitumia sambamba na matumizi mengine ya nishati ikiwemo kuzalisha umeme ili kujenga uchumi wa viwanda."

Akifafanua, Waziri alisema mathalani, takribani asilimia 80 ya gesi inayozalishwa kwa sasa hapa nchini inatumika kuzalisha umeme na kwamba umeme unaozalishwa na gesi asilia kwa Tanzania ni asilimia 57 sawa na megawati 892, akibainisha kuwa huo ni mchango mkubwa sana wa sekta ya nishati kwenye uchumi wa nchi.

Hata hivyo alisema, pamoja na kiasi kikubwa cha gesi kutumika kuzalisha umeme, kiasi kingine kinatumika katika shughuli nyingine mbalimbali ambazo ni pamoja na kuunganisha viwandani, kwenye makazi ya watu na migahawa kwa ajili ya kupikia pamoja na kutumika katika magari.

Katika kuweka msisitizo wa matumizi ya gesi asilia katika magari, Dkt Kalemani alitoa agizo kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati pamoja na watendaji wakuu wa Taasisi zote zilizo chini yake, kuhakikisha magari yote yanayoagizwa kuanzia sasa, yawe ni yale yenye mfumo wa kutumia gesi badala ya petroli na dizeli.

Akizungumzia faida za kutumia gesi asilia kwa shughuli mbalimbali, alisema ni pamoja na utunzaji wa mazingira kutokana na uwepo wa kiasi kidogo cha hewa ya ukaa pamoja na gharama nafuu kwa mtumiaji ambayo inakadiriwa kuokoa asilimia 40 ikilinganishwa na gharama za aina nyingine za nishati.

Kuhusu mipango ya serikali kusambaza gesi asilia kwa matumizi ya kupikia, Waziri alieleza kuwa, mpango huo umeanza kutekelezwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara na Pwani na baadaye mikoa mingine pia itafikiwa.

Alikipongeza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa uamuzi wa kutumia gesi asilia na kuvitaka vyuo vingine na taasisi za umma kuiga mfano huo.

Awali, akitoa taarifa ya utangulizi mbele ya Waziri, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dkt. James Mataragio alisema kuwa uzalishaji wa gesi asilia hapa nchini umefikia wastani wa futi za ujazo milioni 200 kutoka futi za ujazo milioni moja, mwaka 2004 ambapo ndipo uzalishaji wake ulianza rasmi nchini.

Aidha, alieleza kuwa usambazaji wa gesi asilia unafanywa kupitia wakandarasi binafsi na pia kampuni yake tanzu ya GASCO. "Nia yetu ni kuwafikia walaji wengi kadri iwezekanavyo."

Vilevile, aliongeza kuwa, kwa kutumia gesi asilia, viwanda vilivyopo nchini vinapata umeme wa uhakika tofauti na miaka ya nyuma ambapo kulikuwa na changamoto ya umeme kukatika mara kwa mara kutokana na kutegemea chanzo cha maji ambayo wakati wa kiangazi huadimika.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa William Anangisye alisema, kwa kutumia gesi asilia katika maeneo yote isipokuwa uzalishaji wa umeme, Chuo hicho kitaokoa takribani shilingi milioni 479.5 kwa mwaka.

Alisema mradi huo wa kuunganisha gesi asilia chuoni hapo umelenga kuhusisha nyumba za wafanyakazi, migahawa, karakana, maabara za utafiti na kufundishia pamoja na jenereta za dharura.

Profesa Anangisye aliishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kupitia Wizara ya Nishati kwa kutoa fursa ya kupeleka mradi huo wa gesi asilia katika Chuo hicho.

Wengine walioshiriki katika hafla hiyo ni Kamishna wa Petroli na Gesi nchini, Adam Zuberi pamoja na baadhi ya viongozi na wafanyakazi wa Wizara pamoja na TPDC.

Sanjari na tukio hilo la uzinduzi wa matumizi ya gesi asilia UDSM, Waziri pia alikagua baadhi ya makazi ambayo yalikwishaunganishiwa nishati hiyo katika maeneo ya Mwenge Mlalakuwa na Mikocheni.



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (wa tatu kutoka kulia) akisikiliza maelezo ya namna mtambo wa gesi asilia uliopo eneo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam unavyofanya kazi wakati wa hafla ya uzinduzi wa matumizi ya gesi asilia chuoni hapo, Februari 1, 2020.*

# MATUKIO *PICHANI*





*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi rasmi wa matumizi ya gesi asilia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Februari 1, 2020. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) Dkt James Mataragio na kulia ni Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Profesa William Anangisye.*



*Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) Dkt James Mataragio akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi rasmi wa matumizi ya gesi asilia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Februari 1, 2020. Katikati ni Mgeni Rasmi ambaye ni Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na kulia ni Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Profesa William Anangisye.*



*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa William Anangisye akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi rasmi wa matumizi ya gesi asilia katika chuo hicho. Katikati ni Mgeni Rasmi ambaye ni Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) Dkt James Mataragio.*



*Sehemu ya viongozi na wafanyakazi wa Wizara pamoja na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) wakimsikiliza Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), wakati wa hafla ya uzinduzi rasmi wa matumizi ya gesi asilia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Februari 1, 2020.*





*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akikagua migahawa iliyounganishiwa gesi asilia iliyopo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na baadhi ya nyumba zilizounganishiwa nishati hiyo katika eneo la Mwenge Mlalakuwa, Februari 1, 2020.*

# PUMA WATAKIWA KUPELEKA HUDUMA VIJIJINI



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akizungumza akiwa mgeni rasmi katika sherehe za utoaji tuzo na zawadi kwa waendesha vituo vya mafuta vya Puma Energy Tanzania Limited, Februari Mosi, 2020 jijini Dar es Salaam.*

***Veronica Simba – Dar es Salaam***

Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani ameitaka Kampuni ya Puma Energy Tanzania Limited kupeleka huduma zake katika mikoa yote nchini na hasa maeneo ya vijijini.

Amesema kwamba sera ya serikali ni kupeleka nishati za umeme, gesi na mafuta katika maeneo mbalimbali yakiwamo ya vijijini.

Dkt Kalemani aliyasema hayo jijini Dar es Salaam Februari Mosi, 2020 wakati akizungumza akiwa mgeni rasmi katika sherehe za utoaji tuzo na zawadi kwa waendesha vituo vya mafuta vya Puma Energy Tanzania Limited.

"Maagizo yangu ni kwamba mfike mikoa yote nchini ambayo hamjafika ili ipate huduma. Najua hamjafika Katavi, Rukwa, Kigoma, Geita, Mara, Simiyu. Nendeni mikoa hiyo," aliagiza Dkt Kalemani.

Aliongeza, "Sera yetu ni kufikisha nishati vijijini. Nishati hizo ni umeme, gesi na mafuta. Kwa gesi tumefanya vizuri sana na umeme unaendelea kusambazwa vijijini. Ninyi vituo vya mafuta vijijini bado tuko nyuma. Anzisheni vijijini sio mijini."

Alisema si jambo jema kuona wananchi wanabeba mafuta katika madumu au chupa za maji za plastiki huku yakihifadhiwa nyumbani jambo linalohatarisha usalama wa wananchi.

Aidha, aliwaagiza kuongeza ushindani, huku akiwapongeza kwa kutoa ajira 149 za kudumu kwa Watanzania na za jumla takribani 800 kwa wazawa.

Dkt Kalemani alitoa shukrani kwa bodi na menejimenti kwa kusimamia ajira hizo na kuhakikisha Watanzania wengi wanaajiriwa katika kampuni hiyo.

Puma Energy Tanzania limited inamilikiwa kwa asilimia 50 na Serikali ya Tanzania kupitia Msajili wa Hazina na Kampuni ya Puma Investments Limited.

Kutokana na hilo, aliipongeza kwa kutoa gawio kwa Serikali ambalo limekuwa likiongezeka kutoka shilingi bilioni 9.0 mwaka 2018 na shilingi bilioni 11.0 mwaka jana. Aliwataka mwaka huu waongeze kufikia zaidi ya shilingi bilioni 13.

Akizungumzia sekta ya mafuta kwa ujumla, aliwapongeza wadau wote wanaoagiza mafuta kwa pamoja kwa kuiwezesha nchi kuwa na mafuta ya kutosha kila wakati.

Alisema kuna ziada ya mafuta ya dizeli ya siku 28 lita milioni 197, petroli ziada ya lita 97.04 kwa siku 38 na mafuta ya ndege ziada ya lita milioni 30.9 kwa siku 56, hivyo hakuna hofu katika nishati hiyo.

Alimpongeza Rais John Magufuli kwa usimamizi mzuri wa sekta ya nishati na kusimamia uanzishaji wa mfumo wa kuagiza mafuta kwa pamoja.

Pia, Waziri aliwapongeza washindi na wote waliopata zawadi katika sherehe hizo.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Puma Energy Tanzania Limited, Dominic Dhanah alisema hizo ni tuzo za kwanza za aina yake kufanyika nchini.

Dhanah alisema lengo la tuzo hizo ni kutoa hamasa na kuwapa changamoto waendesha vituo hao kutoa huduma bora zaidi kwa wateja wao kote nchini.

"Sisi ni kampuni namba moja kwa ukubwa wa soko tunalolihudumia Tanzania, tukihudumia takribani asilimia 15 ya soko lote Tanzania, lakini pia tukiwa tunatambulika kwa ubora wa huduma zetu, na zaidi ubora wa mafuta yetu na bidhaa zetu nyingine.

"Kwa sasa matamanio yetu makubwa ni kukua zaidi na kuwa kampuni ya kwanza katika soko katika kipengele hiki cha "retail", alisema Dhanah.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Puma Energy, Dkt Selemani Majige alisema wamepokea sifa na changamoto walizopewa na Waziri na kuahidi kuzifanyia kazi ili kuhakikisha kampuni hiyo inazidi kufanya vizuri zaidi na kuchangia zaidi katika pato la serikali kwa kodi na gawio.







*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akiwakabidhi washindi mbalimbali ambao ni waendesha vituo vya mafuta vya Puma Energy Tanzania Limited, tuzo na zawadi katika hafla iliyofanyika Februari Mosi, 2020 jijini Dar es Salaam. Waziri alikuwa Mgeni Rasmi katika sherehe hiyo.*

# KITUO CHA KUPOZA UMEME MLANDIZI KUONGEZEWA UWEZO

*Veronica Simba – Pwani*

Serikali imeuagiza uongozi wa juu wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuanza mara moja ujenzi wa maboresho ya kituo cha kupoza umeme kilichopo Mlandizi, wilayani Kibaha, Mkoa wa Pwani, ili kukiongezea uwezo.

Agizo hilo lilitolewa na Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, aliyetembelea kituo hicho akiwa katika ziara ya kazi mkoani Pwani, Februari 2, 2020.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ziara yake kituoni hapo, Waziri Kalemani alisema ililenga kujionea hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa maboresho husika pamoja na kujiridhisha kuhusu malalamiko ya wananchi kuwa umeme umekuwa ukikatika mara kwa mara na nyakati nyingine unakuwa mdogo usio na nguvu.

"Nashukuru jitihada zimeshaanza za kuagiza vifaa na mashine nyingine zinazohusika. Nimewaagiza TANESCO ujenzi huo uanze kesho (Februari 3) na siyo wiki ijayo kama walivyokuwa wamepanga," alisema.

Akifafanua zaidi kuhusu uboreshaji kituo hicho, Dkt Kalemani alisema unahusisha kufunga mashine mpya yenye uwezo wa megawati 48 za umeme.

Alisema uwezo wa sasa wa kituo hicho ni megawati 48 za umeme, hivyo baada ya uboreshaji wake, zitaongezeka megawati nyingine 48 hivyo kitakuwa na uwezo wa megawati 96.

Waziri alisema, lengo la serikali ni kuhakikisha wananchi wanaopata huduma ya umeme kupitia kituo hicho wanakuwa na umeme wa uhakika muda wote.

"Kwetu sisi TANESCO na Wizara, tumejipanga kila kituo cha kupoza umeme kiwe na ziada ya megawati zisizopungua 50. Kwa hivi sasa kituo hiki kina ziada ya megawati nane katika matumizi, hivyo muda wowote kinaweza kuzidiwa. Tumeona tuchukue tahadhari mapema," alieleza Waziri.

Akizungumzia suala la kukatika umeme mara kwa mara, Waziri Kalemani aliwataka wananchi kuondoa hofu kwani tayari limeshatatuliwa kwa kurekebisha kikata umeme (circuit breaker) ambacho kiliharibika na kufunga kingine kipya.

Hata hivyo, alisema amewaagiza watendaji wa TANESCO kuhakikisha kunakuwa na hifadhi ya vifaa hivyo katika kila kituo cha kupoza umeme nchini, ili kinapoharibika, warekebishe mara moja na kuwaondolea adha wananchi kukaa muda mrefu wakisubiri kifaa kingine kiagizwe na kufungwa.

Awali, katika ziara hiyo, Waziri Kalemani alitembelea kijiji cha Sanzale B, Kata ya Magomeni, wilayani Bagamoyo ambapo aliwasha umeme katika nyumba ya ibada (msikiti) na kuzungumza na wananchi.

Pia, alitembelea kijiji cha Chasimba, Kata ya Yombo, wilayani Bagamoyo, ambapo alilazimika kuchukua hatua kwa wasimamizi mbalimbali wa mradi wa umeme wa 'Peri-Urban' unaoendelea katika eneo hilo kutokana na kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Waziri aliagiza askari wamkamate mkandarasi anayetekeleza mradi huo, ili wakamhoji ni kwanini hatekelezi mradi ipasavyo ambapo tangu mwezi Agosti mwaka jana (2019), hajafanya kitu chochote na amebakiwa na miezi mitatu tu anayotakiwa kukamilisha mradi.

Sambamba na agizo hilo, pia alimtaka mkandarasi huyo kuhakikisha anakamilisha mradi huo ndani ya muda aliopewa kwani serikali haitamwongezea muda.

Pia, aliwaagiza viongozi wa TANESCO kumwondoa aliyekuwa msimamizi wa mradi huo na kumweka mwingine kwani nao hawakutimiza wajibu wao ipasavyo.



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akitoa maelekezo kwa watendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kuhusu uboreshaji wa kituo cha kufua umeme Mlandizi ili kukiongezea uwezo, akiwa katika ziara ya kazi mkoani Pwani, Februari 2, 2020.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, akizungumza na wananchi wa kijiji cha Chasimba, kilichopo Kata ya Yombo, wilayani Bagamoyo, Mkoa wa Pwani alipokuwa katika ziara kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme mkoani humo, Februari 2, 2020.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akizungumza na wananchi wa kijiji cha Sanzale B, Kata ya Magomeni wilayani Bagamoyo (hawapo pichani) mara baada ya kuwasha umeme katika Msikiti wa Kijiji hicho, Februari 2, 2020.*

# DOMESTIC NATURAL GAS PROMOTION PLAN FINALIZED, FIVE REGIONS SET TO BENEFIT AT THE INITIAL PHASE

The Tanzania Ministry of Energy in collaboration with Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC) and Japan International Cooperation Agency (JICA) has finalized the Domestic Natural Gas Promotion Plan (DNGPP).

This Plan which had been conjointly prepared by the threesome over the past three years, maps out natural gas demand from several regions in the country and proposes three key options to dispense natural gas to those regions.

The three options proposed are pipelines, Liquefied Natural Gas (LNG) and Compressed Natural Gas (CNG). Supported by detailed economic analysis, the Plan cogently identifies five regions to start with at the initial phase of Plan implementation. These regions are Dodoma, Morogoro, Arusha, Kilimanjaro and Tanga with Dodoma set as a trial balloon.

Currently, natural gas is utilized in three regions namely Coastal, Dar es Salaam and Mtwara where some



industries, power-plants, households and vehicles are supplied with natural gas. A plan is also afoot to distribute natural gas in Lindi region.

Speaking at the symposium held in Dar es Salaam on 17th January, 2020 which aimed at sharing DNGPP findings with petroleum industry stakeholders, the Tanzania Deputy Minister for Energy used the platform to emphasize that even though the Plan has proposed only five regions to start with, the overarching goal is to supply natural gas to all regions in the country as National Energy Policy, 2015 requires.

Upon explaining the

| | DOMESTIC DEMAND | | | | | | | | | | | EXPORT DEMAND | | TOTAL |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | Petrochemicals | | | | | | | | |
| USER | Electricity | Households | Institutions | CNGV | Industries | *Fertilizer/ Ammonia* | *Methanol* | *GTL* | *DME* | *MTG* | Iron and Steel | LNG | Pipeline | |
| Demand (TCF) | 9.0 | 0.5 | 0.2 | 0.6 | 3.8 | 0.7 | 1.2 | 1.9 | 0.3 | 0.5 | 1.1 | 11.7 | 3.2 | 34.6 |
| **TOTAL (TCF)** | | | | | | | | | | | ***19.7*** | | ***14.9*** | **34.6** |

benefits accrued from using natural gas in the country, the Deputy stressed; "Natural gas contributes 57% in the country's electricity mix. This is to say, electricity generated from natural gas is 892.72 megawatts out of 1,602.31 megawatts, total installed capacity.

Besides, the country has saved over USD 13.048 Billion from when it started using natural gas in 2004 up to date. Generally speaking, the contribution of natural gas to the economy and the environment is significant considering the fact that natural gas is relatively cheaper and environmentally friendlier than some other sources of fuel".

The DNGPP complements the already existing Natural Gas Utilization Masterplan (NGUMP) which was first released to public in 2016. This 30 year-long Masterplan (2017 to 2045) allocates quantities of natural gas required to satiate domestic demand and the quantities for export market as indicated in the figure below. TCF (Trillion Cubic Feet) CNGV (Natural Gas Vehicle) GTL (Gas To Liquid) DME (Dimethyl Ether)

If DNGPP is put into implementation Tanzania will see a surge in natural gas consumption, as a result, more benefits will be reaped from county's natural gas resource.

**Article by Ebeneza Mollel, Energy Geologist, Tanzania Ministry of Energy, ebenezamollel@yahoo.com**

# MATUKIO PICHANI



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akikagua migahawa iliyounganishiwa gesi asilia iliyopo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na baadhi ya nyumba zilizounganishiwa nishati hiyo katika eneo la Mwenge Mlalakuwa, Februari 1, 2020.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, akikata utepe kabla ya kuwasha umeme katika Msikiti wa Kijiji cha Sanzale B, Kata ya Magomeni, Wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani, Februari 2, 2020.*